
Jumatatu Oktoba 5, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580359
The Guardian digital
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



**MOTO** waunguza bweni la sekondari Manyara

UKURASA 4



**SERIKALI** yarejesha mali za ushirika zilizouzwa kiujanja

UKURASA 4

Wengi Dar wana uzito kupindukia

UKURASA 10



# Ushirikiano rasmi

**NI** wa CHADEMA, ACT-Wazalendo kuelekea Oktoba 28...*Endelea Uk. 2*

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitoa tamko la kumuunga mkono mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT- Wazalendo, Maalim Seif Hamad na kumuengua mgombea wa chama chao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mlinzi wa bilionea Laizer akutwa kauawa kinyama

UKURASA 3



## Maalim Seif aibuka na vipaumbele 8 miaka 5

UKURASA 2


# FURSA

Mawakala wa uuzaji Magazeti







Kampuni ya **THE GUARDIAN LIMITED.**
Inakutangazia ya kuwa inatafuta mawakala wa wauzaji wa magazeti yake nchi nzima.kama unafahamu Biashara , au umeshawahi kufanya biashara unakaribishwa unatakiwa uwe na vitu vifuatavyo;

- Amana ambayo itafafanuliwa kutokana na idadi ya magazeti utakayohitaji
- Uwe na wauzaji (Vendors)
- Kitambulisho cha uraia
- Barua ya Mdhamini.
- Barua ya utambulisho wako kutoka kwa Mwenyekiti wa Serikali ya mitaa unapoishi.
- Barua ya utambulisho ya Mdhamini wako kutoka kwa Mwenyekiti wa serikali ya mitaa
- Picha 2 za Muombaji

Hii ni fursa ya kupata faida kubwa kwa kila nakala moja ya gazeti utakayouza.

Kwa Maombi na Ufafanuzi zaidi Wasiliana nasi

Meneja Usambazaji na Masoko
Mikocheni Light Industrial Area
S.L.P 31042, Dar es Salaam, Tanzania
Namba :+255716500500
Barua Pepe:circulation@guardian.co.tz
Mwisho wa Maombi ni 13 Oktoba 2020


**MICHEZO** NYOTA WAGENI YANGA WAENDELEA KUNG'ARA UK. 23

MAONI, KATUNI UK. 6


Fursa kwa Wagombea! 2020

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE

# Maalim Seif aibuka na vipaumbele 8 miaka 5

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha ACT- Wazalendo, kimezindua Ilani ya Uchaguzi wa Zanzibar ya Mwaka 2020-2025, iliyojikita katika maeneo manane ya kipaumbele yanayotarajiwa kugharimu Sh. trilioni 12 katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Ilani hiyo ilizinduliwa rasmi jana visiwani hapa na Mwenyekiti wa chama hicho na mgombea urais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, aliyeahidi kuleta haki na usawa pamoja na maisha ya raha na furaha kwa wananchi.

"ACT-Wazalendo itahakikisha inawaondoa wanawake na vijana katika dimbwi la umaskini kwa kukukuza vitega uchumi na kuongeza mianya ya ajira.

"Tutawapunguzia wananchi mzigo na kuinua hali yao ya maisha. Kikubwa na jambo muhimu la kufanya ni Wazanzibar kuchukua uamuzi sahihi, na uamuzi sahihi ni kuichagua ACT-Wazalendo, ili kuifanya Zanzibar kuwa sehemu ya raha na furaha," alisema.

VIPAUMBELE VINANE

Akiwasilisha muhtasari wa ilani hiyo wakati wa uzinduzi wake jana, Mjumbe wa Kamati ya Ilani, Othman Masoud Othman, alisema chama hicho kama kitapewa ridhaa ya kuongoza serikali, kitatumia Sh. trilioni 12 kuwekeza kwenye maeneo manane ya kipaumbele ndani ya miaka mitano.

Aliyataja maeneo hayo ya kipaumbele yanayohitaji fedha nyingi kuwa ni pamoja na mradi wa elimu, hasa utanuzi wa elimu ya msingi na sekondari kutokana na kasi ya uongezeko la wananfunzi, chama hicho kikikusudia kujenga vyuo vya ufundi, kufadhili elimu ya juu kwa Wazanzibar na kuboresha vyuo vya ualimu.

Masoud alisema kipaumbele cha pili ni kuchangia hifadhi ya jamii kwa watu walio nje ya sekta rasmin, ili kila Mzanzibar awe kwenye mfumo wa hifadhi ya jamii na kupata fao la bima ya afya.

Alisema eneo la tatu litakalotiliwa mkazo na ACT-Wazalendo, ni ujenzi wa hospitali za rufani kila mkoa, maabara ya kimataifa na vituo vya utafiti Unguja na Pemba.

Kipaumbele cha nne ni utekelezaji wa mpango mkakati wa maji kwa kila Mzanzibar na eneo la tano ni ujenzi wa barabara mpya katika maeneo mkakati kilomita 250, ili kuchochea utalii na biashara.

Kwa mujibu wa Masoud, vipaumbele vingine ni ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Unguja na ujenzi wa Uwanja wa Ndenge Pemba pamoja na mradi wa uzalishaji wa umeme megawati 100.

Kipaumbele cha nane ni mradi wa bandari kubwa za kisasa, moja Pemba na moja Unguja pamoja na kituo cha mizigo Afrika Mashariki.

**VYANZO VYA MAPATO**

Katika wasilisho lake hilo, Masoud aliyewahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Zanzibar, alisema chama hicho kinatarajia kupata fedha kutokana na uwekezaji wa mitaji ndani ya Zanzibar na uwekezaji wa skimu ya hifadhi ya jamii kama uwekezaji wa skimu ya muda mrefu.

Alivitaja vyanzo vingine vya mapato kuwa ni madeni ambayo Serikali ya Zanzibar inadai pamoja na fedha za malimbikizo ya Zanzibar kutoka fedha za mapato ya Muungano.

Vingine ni uwekezaji wa ubia kati ya sekta binafsi na serikali (PPP), kodi na mapato ya ndani, misaada na mikopo kutoka nje, Masoud akisisitiza kwamba hilo litawezekana tu ikiwa watarejesha mamlaka ya Zanzibar katika ushirikiano wa kimataifa kimaendeleo na hivyo kupokea misaada na mikopo moja kwa moja.

Alisema kutekelezwa kwa vipaumbele hivyo kutaboresha huduma za jamii kama afya, maji, elimu na kuwa na siasa zinazowafikia wananchi wote na Zanzibar kujitegemea kinishati.

Pia kutaimarisha miundombinu wezeshi kwa uchumi wa visiwa hivyo, kutaifanya Zanzibar kuwa kituo cha biashara, fedha na uwekezaji katika eneo la maziwa makuu, kutaendeleza sekta za utalii, mafuta na gesi asilia na kuchochea kilimo cha mapinduzi, uvuvi na ufugaji.



Mgombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, akizindua Ilani ya uchaguzi wa Zanzibar ya chama hicho 2020-2025 mjini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ushirikiano CHADEMA, ACT-Wazalendo rasmi

**Na Elizabeth Zaya**

KAMATI Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), imekubali kushirikiana na Chama cha ACT-Wazalendo kwa ngazi za udiwani, ubunge na urais.

Aidha, chama hicho kimeziagiza kamati za kiufundi za mikoa, majimbo na kata kujadili na kukubaliana mgombea mwenye nguvu katika kila ngazi na kukubali kuachiana na ACT-Wazalendo, na kwamba mchakato huo ufanyike kwa haraka.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusiana na uamuzi wa kamati hiyo, Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, alisema kauli zinazotolewa na mgombea urais wa chama hicho, Tundu Lissu, juu ya ushirikiano si zake pekee yake bali zina baraka za chama.

Alisema kwa Zanzibar wameshakubaliana kumuunga mkono Maalim Seif Hamad na mgombea wa CHADEMA, Said Mohamed kwa hiari yake amekubali kumuunga mkono mgombea wa ACT-Wazalendo.

**'USHIRIKIANO HAUKATAZWI'**

"Sisi tuko tayari endapo ACT-Wazalendo watamuunga mkono mgombea wetu wa urais kama ambavyo matamko yamekuwa yakitolewa na baadhi ya viongozi wao, wao ndio watazungumza hili kwa sababu bado hawajatoa tamko rasmi," alisema Mbowe.

Alisema ushirikiano wanaouzungumzia wao ni wa uhusiano binafsi ambao haukatazwi kokote na hakuna kosa la kisheria wala kikanuni.

"Tumesikia matamko ya viongozi kadhaa wakizungumza dhana ya ushirikiano wa vyama, na tumemsikia msajili wa vyama vya siasa akisema muda umepita, haya ni mambo ya kusikitisha sana. Kumshawishi rafiki yangu aniunge mkono ni uamuzi binafsi na uhusiano binafsi," alifafanua Mbowe.

"Vyama pingamizi vya upinzani kama UDP na TLP walipojsema wanamuunga mkono mgombea wa CCM, Msajili alikuwa hana maneno ya kuzungumza, lakini alivyoona kwamba ACT-Wazalendo na CHADEMA alitupa barua," alisema.

**ZITTO AFUNGUKA**

Alipoulizwa na NIPASHE kuhusiana na kikao cha ushirikiano kilichokuwa kifanyike Oktoba 3, mwaka huu, Zitto alisema bado wanaendelea na mazungumzo na watakamilisha hivi karibuni.

Aidha, akiwa Jimbo la Mhambwe mkoani Kigoma Oktoba mosi mwaka huu, Zitto alisema; "Lengo letu ni kumshinda Dk. John Magufuli, tukienda vibaya tunazigawa kura, anapita katikati, maelekezo yetu, chagueni mgombea ambaye mnamuona ana nguvu za kumshinda Magufuli."

**LISSU KUFANYA KAZI ZA CHAMA**

Aidha, Mbowe alisema kamati hiyo iliamua kuwa mgombea wa urais wa chama hicho, Lissu, asiendelee na kampeni kama alivyozuiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), badala yake atapangiwa ratiba ya kazi za chama kama Makamu Mwenyekiti.

Mbowe alisema tayari chama kimempangia majukumu mengine ya kisiasa na kijamii mgombea huyo wa urais wa CHADEMA atakayofanya kwa kipindi chote atakachokuwa hafanyi kampeni.

"Lissu siyo tu ni mgombea urais, bali ni Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, kwa hiyo ataendelea kufanya kazi nyingine za kijamii na kisiasa kama kiongozi wa chama na ratiba ya shughuli hizo atakazozifanya itatolewa (kesho) leo asubuhi, NEC haiwezi kumzuia kufanya shughuli za kijamii na za chama," alisema Mbowe.

**KUFUNGUA KESI MAHAKAMANI**

Kwa mujibu wa Mbowe, chama hicho kinatarajia kufungua kesi mahakamani kulalamikia hatua zilizochukuliwa na NEC dhidi ya mgombea wao.

"Tumeelekeza kwa hati ya dharura kufungua kesi mahakamani kupinga uamuzi huu wa NEC, tunajua kesi inaweza isihukumiwe kwa wakati, lakini inabidi tuweke kwenye rekodi mambo," alisema Mbowe.

**MAMBO MANNE WAKUBALI MATOKEO**

Mbowe alitaja mambo manne ya kuzingatia ili chama hicho kikubaliane na matokeo yatakayotangazwa kwamba ni mawakala wa CHADEMA wasinyimwe fursa ya kuapishwa, wasizuiwe kwa njia yoyote kwa visingizio vyovyote katika vituo vya kupigia kura kuanzia asubuhi.

La tatu, wapewe nakala za matokeo ya kura za rais, wagombea wa ubunge na madiwani na wasimamizi wa uchaguzi kutangaza matokeo halali kama kura zilivyopigwa.

## HABARI KITAIFA

# Sera yaja kupunguza gharama za nyumba

**Na Munir Shemweta**, IRINGA

WAKATI leo ni maadhimisho ya Siku ya Makazi Duniani, serikali iko katika hatua mbalimbali za kuandaa sera ya nyumba ili kukabiliana na changamoto zilizopo kwenye sekta hiyo sambamba na kuwezesha mazingira ya upatikanaji wa nyumba za gharama nafuu.

Akitoa salamu za Siku ya Makazi Duniani mkoani Iringa jana kuelekea maadhimisho hayo leo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema sera hiyo itatoa dira ya uendelezaji wa sekta ya nyumba nchini.

Aliongeza kupitia sera hiyo juhudi zitaelekezwa katika kubuni mbinu mbalimbali za kuwawezesha wananchi wa kipato cha chini kupata nyumba bora.

Aidha, Waziri Lukuvi alisema serikali imeanzisha miradi na mifuko mbalimbali ya kusaidia kuwezesha maendeleo ya sekta ya nyumba nchini, na kubainisha kuwa kupitia mradi wa mikopo ya nyumba na taasisi za fedha zimekuwa zikipatiwa mitaji kwa ajili ya kutoa mikopo ya nyumba.

Kwa mujibu wa Lukuvi, hadi sasa serikali imetoa mikopo isiyopungua Sh. bilioni 438.58 na wananchi wapatao 5,460 wamenufaika na mikopo kwa utaratibu huo.

Sambamba na hilo, Lukuvi alisema serikali inafanya kazi kwa karibu na taasisi mbalimbali za kifedha kwa kuimarisha vyama vya ushirika ili kuhakikisha fedha zinapatikana kwa makazi ya watu wa kipato cha chini na kubainisha kuwa mikopo midogo midogo imekuwa ikisaidia ujenzi wa awamu kwa watu wa kipato cha chini.

"Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa taasisi zisizo za kiserikali (NGO) katika kuboresha makazi na baadhi ya taasisi hizo zimekuwa zikishiriki katika uboreshaji wa nyumba za makazi yasiyokuwa rasmi,'' alisema Lukuvi.

Aidha, Lukuvi alisema Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) itaendelea kutekeleza miradi ya urasimishaji nchini kwa kutambua miliki hatua kwa hatua ili kuyaweka maeneo yenye makazi holela huduma za kiuchumi na kijamii kupitia mpango shirikishi.

Kadhalika, Lukuvi alisema, wizara yake iko katika maandalizi ya kufanya sensa ya nyumba ili kutambua idadi kamili ya nyumba na kusaidia kubaini uhaba na hali ya nyumba na kusisitiza kuwa matokeo ya sensa hiyo yatasaidia kuandaa mipango mikakati ya maendeleo ya nyumba.

# Mlinzi wa bilionea Laizer akutwa kauawa kinyama

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MFANYAKAZI wa mgodi wa madini ya Tanzanite unaomilikiwa na Bilionea Saniniu Laizer, Manase William (47), mkazi wa Ilkiding'a wilayani Arumeru, Mkoa wa Arusha, ameuawa kinyama na watu wasiojulikana na mwili wake kuegeshwa pembezoni mwa mgodi.

Familia ya marehemu imesema imeshtushwa na tukio hilo, na kuliomba Jeshi la Polisi mkoani Manyara kufanya uchunguzi wa kifo hicho chenye utata baada ya taarifa za awali kudai kuwa aliuawa na majambazi, jambo walilodai kuwa si kweli.

Akiongea kwa masikitiko baada ya mwili wa marehemu kufanyiwa uchunguzi katika Hospitali ya Mkoa Mount Meru jana, kaka mkubwa wa marehemu, Peter William, alidai kuwa Manase aliuawa Septemba 27, mwaka huu katika mgodi, 'block D' unaomilikiwa na mchimbaji mdogo, Saniniu Laizer, na mwili wa marehemu kuegeshwa kwenye eneo lake la kazi huku taarifa zikieleza kuwa ameuawa na majambazi.

"Tulipata taarifa kuwa ndugu yetu ameuawa na majambazi, lakini tulipoenda eneo la tukio tulitilia shaka tukio hilo kwani hakuna mahala ambapo majambazi wamevunja au kupora, pia marehemu hakuuawa eneo la tukio ila mwili wake ulipelekwa pale ndio maana tumegoma kuuzika ili ufanyiwe uchunguzi," alidai.

Alidai kuwa baada ya mwili wa marehemu kufanyiwa uchunguzi taarifa zilionyesha kwamba marehemu alikutwa na majeraha kadhaa kichwani yaliyoonyesha kupigwa na kitu kizito chenye ncha kali na kuvuja damu nyingi zilizosababisha kifo chake.

"Tunalitaka Jeshi la Polisi lifanye uchunguzi wa kina ili sheria ichukue mkondo wake kwani ndugu yetu hakuuawa na majambazi bali ameuliwa kikatili," alidai Peter.

Kaka mwingine wa marehemu, Efatha Mollel, alidai baada ya kushuhudia mwili wa mdogo wake na taarifa za daktari, wameridhika kwamba ndugu yao aliuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani na kuliomba Jeshi la Polisi kuchukua hatua kali kwa wahusika ili iwe fundisho kwa mauaji ya kutatanisha yanayojitokeza Mererani.

Alidai kuwa mdogo wake alikuwa ameajiriwa katika mgodi wa Saniniu Laizer na amefanyakazi kwa muda mfupi wa miezi miwili na kwamba taarifa za awali kuwa aliuawa na majambazi hazina ukweli wowote kwa kuwa hakuna mahala palipovunjwa ama kuporwa katika tukio hilo.

"Baada ya mwili wa ndugu yetu kufanyiwa uchunguzi tumeridhika na taarifa ya daktari tunajipanga kufanya mazishi nyumbani kwake Ilikiding'a na baada ya hapo ndugu watakaa na kutoa tamko," alisema Mollel.

Naye Meneja wa mgodi huo, Kiria Laizer, alisema tukio hilo limewasikitisha na wameliomba Jeshi la Polisi kuchukua hatua ili kubaini ukweli wa tukio hilo na kuahidi kushirikiana na ndugu wa marehemu katika mazishi ya marehemu.

Akizungumzia tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Paul Kasabago, alisema kuwa Jeshi la Polisi linawashikilia watu saba wakiwamo wafanyakazi wa mgodi wa Saniniu Laizer, wakihusishwa na tukio hilo la mauaji.

Alisema uchunguzi bado unaendelea na upelelezi utakapokamilika watafikishwa mahakamani.



Mgombea wa urais kupitia Chama cha ADC, Queen Cuthbert Sendiga, akihutubia wananchi, wavuvi na wafanyabiashara wa soko la samaki Bagamoyo, mkoani Pwani juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgombea urais ADC aahidi wavuvi fursa

**Na Boniface Gideon,** PWANI

MGOMBEA urais kupitia Chama cha ADC, Queen Sendiga, amewaahidi wavuvi fursa ikiwa atachaguliwa.

Alitoa ahadi hiyo jana wilayani Bagamoyo mkoani Pwani alipokutana na kuzungumza na wavuvi ikiwa ni sehemu ya mikutano ya kampeni.

Akizungumza katika viwanja vya soko la samaki mjini Bagamoyo, Sendiga alisema Ilani ya chama hicho imeweka vipaumbele kwa ajili ya sekta ya uvuvi.

"Wavuvi ni kundi kubwa sana ambalo ukiwatengenezea maisha mazuri, mipango na taratibu tunatengeneza ajira nyingi sana za kutosha na zenye uhakika kwa sababu mvuvi akiumwa siku tatu ama siku nne hawezi kwenda kuvua tena," alisema.Alisema chama chake kimejipanga kuboresha maisha ya mvuvi kwa kuwawezesha kuwapatia elimu ya uvuvi, zana na mikopo yenye riba nafuu.

"ADC chini ya uongozi wangu kwa miaka mitano tunaenda kuhakikisha mvuvi wa kitanzania anaenda kuwa mvuvi bora, mwenye kupatiwa elimu juu ya shughuli zake za uvuvi, mwenye kupatiwa vitendea kazi bora na kuondolewa tozo zisizoendana na uwezo wake wa kuvua, na cha mwisho anaenda kuongezewa thamani ya bidhaa zake zinazotoka baharini ili iweze kumkwamua kutoka alipo kimaisha " alisema Sendiga.

Aliongeza kuwa wavuvi kwa sasa wamekuwa wakipitia changamoto mbalimbali katika shughuli zao ikiwamo kuchomewa nyavu, na kwamba akiingia madarakani ataziondoa zote ili wavuvi wafanye shughuli zao bila vikwazo vyovyote.


IN THE RMS COURT / DISTRICT COURT OF MOSHI
AT MOSHI

MISC.CIVIL APPL/CASE/MATRIMONIAL CAUSE NO.17 OF 2019

COURAGE WORLDWIDE WC
(CWW)............................................PLAINTIFF/APPL.

VERSUS

SECAO BUILDERS CO- LTD & THE BOARD OF REGISTERED................................DEFENDANTTRUSTEES OF MKOMBOZI CENTRE FOR STREET CHILDREN & INDEPENDENT ANGENCIES & COURT BROUKER LTDNOTICE OF MENTION/HEARING.

TO: THE BOARD OF REGISTERED STUSTED OF MKOMBOZI CENTRE FOR STREET CHILDREN

Take Notice that the above case has been fixed for hearing/mention/ruling judgement in the RMS court at Moshi on 15th the day of October 2020 at 9:00am Oclock in the forenoon.
You may appear in person or by advocate of agent dully authorized to do so and you are directed to produce on that day of document under which you intend to rely in support of your case.
TAKE FURTHER NOTICE that, default of your appearance on that day before mention the court will proceed with the matter in your absence.
A copy of the petition of appeal, Judgement and decree are attached hereto.
Given under my hand and seal of this Court this 2 day of October ,2020

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE I /C
MOSHI

115929802



KUPOTEA KWA PASPORT



115929702

DICKSON ELIAFIE LEMA
Mtajwa hapo juu amepotelewa na passport yenye no, TAE 222513 iliyotolewa na ofisi ya uhamiaji October 2019 Dar Es Salaam. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
KL/MOS/RB/700049/2020

# DC aziagiza TAKUKURU, Polisi kuchunguza SACCOS

**Na Francis Godwin,**
IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kumkamata na kumchunguza meneja wa Iringa Cummunity SACCOS, anayetuhumiwa kuhujumu SACCOS hiyo iliyopo Miyomboni mjini Iringa.

Aidha, ameagiza TAKUKURU kuchukua nyaraka zote za uendeshaji wa SACCOS hiyo, kwa ajili ya uchunguzi ili kujua waliohusika kuhujumu na kuiyumbusha.

Kasesela alifikia uamuzi huo juzi baada ya wanachama zaidi ya 50 wa Iringa Community Saccos kuandamana kwenda ofisini kwake kulalamikia uendeshaji wa ovyo wa chama hicho.

Alisema kuwa kwa malalamiko ambayo amepokea kutoka kwa wanachama hao na kujiridhisha kwa maelezo ya mwenyekiti wa Saccos hiyo amebaini kuna tatizo mahali.

"TAKUKURU na Jeshi la Polisi shirikianeni kufanya uchunguzi iwapo itabainika kuna uchakachuaji wa fedha za wanachama basi hatua za kisheria zichukuliwe ili fedha za wanachama hao zirejeshwa, kazi hii ifanyike ndani ya siku saba," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa SACCOS hiyo, Khamisi Kihemba, alisema kuwa ilianza kama kikoba na baada ya kuona wanachama wamefika zaidi ya 3000 waliamua kuanzisha Saccos baada ya kushauriwa na maofisa ushirika.

Alisema kutokana na wanachama wengi kutaka kujitoa kuendelea na SACCOS walianza kuwarejeshea fedha wanachama wanaojitoa na kuwa kuna mikopo zaidi ya milioni 100 wamekopesha nje na haijarejeshwa.



Mgombea mwenza wa kiti cha urais kwa tiketi ya CCM, Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, akiinadi Ilani ya Uchaguzi ya chama ya 2020/25 kwa wanachama wa chama hicho na wananchi wa Nzega, mkoani Tabora jana. **PICHA: OMR**

# Serikali yarejesha mali za ushirika zilizouzwa kijanja

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imerejesha mali za ushirika mkoani Kilimanjaro, zikiwamo nyumba tatu na magari matatu yaliyouzwa kinyemela na wajanja wachache, kwa bei ya kutupwa ili kujinufaisha kiuchumi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alisema mpango wa sasa wa serikali ni kuhakikisha kila aliyepora mali za ushirika nchini, anachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kurejesha kwa nguvu mali hizo.

Kusaya alieleza mpango huo jana, wakati akikabidhi magari matatu ya kiwanda cha kukoboa kahawa cha Tanganyika Coffee Curing Co. Ltd (TCCCo), yaliyokombolewa kutoka kwa matajiri waliouziwa kinyemela magari hayo.

Magari hayo ni Land Cruiser hardtop, lenye namba za usajili T 187 ACD, lililokuwa likifanya biashara ya utalii mkoani Arusha, Land Cruiser GX, T 199 CD na lori la mizigo aina ya Fiat, lenye usajili T 215 ACD.

"Hatutakubali kama serikali watu wachache wapole mali za ushirika, watazitapika na zitarudi mikononi mwa wana ushirika. Niwasihi sana wanachama na viongozi wa vyama vya ushirika kote nchini, mlinde na kutunza mali za ushirika zisichukuliwe tena," alisema.

Kabla ya makabidhiano hayo, Mwenyekiti wa Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika mkoani Kilimanjaro, John Boshe, alisema ubadhirifu wa mali hizo za ushirika ulitokana na usimamizi mbovu wa viongozi waliopewa dhamana ya kuzisimamia.

Alisema jambo hilo ndilo lililosababisha vyama vingi vya ushirika, ikiwamo kiwanda cha kukoboa kahawa kushindwa kufanya kazi, licha ya kuwa na mitambo iliyonunuliwa kwa gharama kubwa.

Katika hafla hiyo ya makabidhiano, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alimwomba Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, kuamuru kufanyika upya mapitio ya uamuzi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Moshi kuwaachia huru vigogo wa ushirika mkoani hapa, waliokuwa wakiabiliwa na kesi mbili za uhujumu uchumi wanazodaiwa kusababisha hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 4.9.

Dk. Mghwira alieleza kutoridhishwa na uamuzi huo wa mahakama na kutaka Wizara ya Kilimo, kuchukua hatua zaidi kwa kuiomba kufanya mapitio upya kuhusu uamuzi wake.

# Moto waunguza bweni la sekondari Manyara

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

JINAMIZI la shule nchini kuungua linaendelea kuipasua kichwa serikali, baada ya Shule ya Sekondari ya Oljoro namba 5 iliyopo Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara kuungua moto, huku chanzo chake kikiacha maswali.

Shule hiyo ni ya mchanganyiko, lakini bweni lililoteketea ni la wasichana, kwa mujibu wa Jeshi la Polisi.

Jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi, Paul Kasabago, alithibitisha kuungua kwa shule hiyo.

Kwa mujibu wa Kasabago, tukio hilo lilitokea Oktoba 2 mwaka huu, majira ya saa 6:00 mchana, wakati wanafunzi wanapata chakula cha mchana.

Aidha, alisema vifaa vya wanafunzi hao vimeteketea kwa moto hasa magodoro.

"Mimi niwasifu sana wanafunzi, walimu na majirani kwa kuuzima moto huo kiasi kikubwa na kusaidia jengo kusalimika," alisema Kasabago.

Kamanda huyo alisema wanaendelea na uchunguzi licha ya kwamba wamebaini shule hiyo haina miundombinu ya umeme, labda wanatumia nishati ya jua, hivyo wamebaki na maswali moto umetoka wapi.

"Madirisha yao yako juu sana kwa hiyo ni vigumu kufanya hujuma, tumeangalia hawana pasi ya umeme, tumeuliza wana pasi ya mkaa wakasema ipo ila ni mbovu," alieleza.

Kasabago alifafanua kuwa ingekuwa ni wavulana wangesema ni watundu labda wamevuta sigara ndio maana umeibuka moto huo.

Vile vile alisema Jeshi la Polisi mkoani humo limeshatoa maelekezo kwa shule zote kuwa waweke walinzi usiku na mchana.

"Na ikiwezekana mabweni yawe yanawekewa watu maalum wa kuyalinda na ni lazima shule zote ziweke mkakati wa kulinda shule zao," alisisitiza.

Alisema ni lazima wakuu wa shule wafuate maelekezo yaliyotolewa na Jeshi la Polisi na ameagiza shule hiyo iliyoungua kujenga uzio, ili iwe rahisi kudhibiti wahalifu wanaochoma shule.

Matukio ya moto katika shule ni changamoto ambayo bado serikali inaitafutia majibu kutokana na kufululiza.

Hivi karibuni wanafunzi 10 katika Shule ya Msingi ya Wavulana ya Byamungu Islamic iliyopo Kyerwa mkoani Kagera walikufa kwa moto Septemba 14, mwaka huu, baada ya shule kuteketea kwa moto.

HABARI KITAIFA

# Udhibiti ugonjwa wa mdondo waonyesha matokeo chanya

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya chanjo ya Kibaha mkoani Pwani imeanza kuonyesha matokeo chanya baada ya kufanikiwa kudhibiti ugonjwa wa mdondo kwa asilimia 95.

Akizungumza na waandishi wa habari na wahariri wa vyombo vya habari waliotembelea katika taasisi hiyo kushuhudia shughuli za utengenezaji wa chanjo za kudhibiti magonjwa ya mifugo zinazofanywa na taasisi hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (sekta ya Mifugo), Profesa Elisante Ole Gabriel, alisema mafanikio hayo ni kwa wafugaji waliozingatia kuchanja kuku wao mara tatu kwa mwaka kama inavyoelekezwa na wataalamu wa mifugo.

"Taasisi ya chanjo Kibaha ilipoanza ilikuwa inazalisha aina moja ya chanjo stahimilivu joto ya 1-2 maarufu kwa jina la 'chanjo matone' inayokinga dhidi ya ugonjwa wa mdondo ambayo imeleta mafanikio makubwa kwa kudhibiti ugonjwa huo nchini kwa zaidi ya asilimia hususani kwa wafugaji wanaozingatia," alisema Profesa Gabriel.

Pia alisema kwamba kwa sasa taasisi hiyo imefanikiwa kuongeza uwezo wa kuzalisha aina sita za chanjo na kati ya hizo, tano ni kwa ajili ya ng`ombe, mbuzi na kondoo ambazo zinakinga magonjwa hatari ya kimeta, chambavu, homa ya mapafu ya ng'ombe na ugonjwa wa kutupa mimba.

Alisema lengo la wizara ni kufanikisha kuzalisha chanjo aina 13 kwa ajili ya kukinga magonjwa 13 ya kimkakati ambayo ndiyo kikwazo kikubwa katika ustawi wa afya ya mifugo nchini.

"Lengo ni kuuleza umma wa Watanzania juu ya mageuzi makubwa katika Sekta ya Mifugo yanayolenga kuwa na sekta endelevu yenye tija katika kuboresha maisha ya wafugaji na kuchangia pakubwa katika pato la taifa," alisema Profesa Gabriel.

Alitoa wito kwa halmashauri zote nchini kununua na kutumia chanjo zinazozalishwa na taasisi hiyo katika kampeni za uchanjaji kama ilivyoelekezwa kwenye kanuni za chanjo na uchanjaji za mwaka 2020.

Alisema taasisi hiyo ipo chini ya Wakala wa Maabara ya Veterinari ambayo imekabidhiwa jukumu la kuboresha afya ya mifugo nchini kwa kutafiti, kutengeneza na kusambaza teknolojia za kudhibiti magonjwa ya mifugo.

"Taasisi hii ilianzishwa mwaka 2012 kwa lengo la kupanua shughuli za uzalishaji wa chanjo za mifugo ambazo awali zilifanywa kwa kiwango kidogo na Maabara Kuu ya Mifugo Temeke. TVI imejengwa katika eneo hili lenye ukubwa wa hekta 1037, eneo ambalo linaruhusu uwekezaji wa kiwango chochote katika uzalishaji wa chanjo ikiwa ni pamoja na kujenga maabara za kuzalisha chanjo ambazo hazihitaji kuwa karibu na makazi ya watu," alisema Profesa Gabriel.

"Lakini eneo hili linaruhusu kufanyika kwa shughuli za utafiti ambazo ndio msingi wa kutengeneza chanjo mpya au kuboresha chanjo zilizokwisha kuzalishwa kulingana na teknolojia inavyobadilika."

Mtendaji Mkuu wa wakala huyo, Dk. Huraha Mramba, alisema wakusudia kuboresha miundombinu ya uzalishaji na usambazaji wa chanjo ikiwamo kununua mashine za vifaa zaidi ili kupanua uzalishaji wa kufikia chanjo 13 za kimkakati zilizoainishwa na wizara.

Aliyataja magonjwa ya mifugo ambayo ni kikwazo katika uzalishaji wa mifugo nchini ni mdondo, kimeta chambavu, 'brucellosis' ambapo alisema lengo ni kupanua wigo wa aina za chanjo zinazozalishwa kwa kuongeza chanjo tatu za kimkakati homa ya mapafu, sotoka ya mbuzi na kichaa cha mbwa.




Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano Vodacom Tanzania Plc, Jacquiline Materu (kulia), akipanda mti na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kikwe, iliyopo Tengeru mkoani Arusha jana, ikiwa ni sehemu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi (SDG 13), wakati wa mkutano uliojadili nafasi ya vijana katika kuwaandaa kwa nyakati zijazo, ulioandaliwa na Shirikisho la Vijana la Umoja wa Mataifa (YUNA) na kudhaminiwa na kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tani 774 za korosho zakusanywa kwa wakulima

**Na Said Hamdani,** LINDI

TANI 774 za korosho zimekusanywa kutoka kwa wakulima mbalimbali na kufikishwa Chama Kikuu cha Ushirika cha Lindi Mwambao, kupitia vyama vya msingi na ushirika (Amcos) kwa muda wa siku nne.

Idadi hiyo imetolewa na Ofisa Masoko wa Chama hicho, Gloria Makere, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake iliyopo Barabara ya Kawawa mjini Lindi.

Alisema korosho hizo zimekusanywa kuanzia Septemba 28 hadi Oktoba 01 mwaka huu, kupitia vyama vya msingi vya ushirika (18) kati ya (54) vilivyo chini ya mwamvuli wa Chama Kikuu cha Lindi Mwambao.

Aidha, hakufafanua kiasi kilichokusanywa kwa kila chama na kwamba tayari zimehifadhiwa katika maghala makuu manne ya Bucco, Manispaa ya Lindi, Mnolela, Mtama na Nangurukuru Wilaya ya Kilwa.

Makere ametaja changamoto zilizojitokeza kabla ya msimu kuanza ni upatikanaji wa vifungashio (Magunia) kwa ajili ya kuhifadhia korosho kutoka kwa mzabuni aliyechukuwa tenda ya kuagiza na kusambaza kwenye vyama husika.

"Msimu ulipoanza tulikuwa na vifungashio (magunia 3,000) tu, na ndivyo tumeanza nazo ikizingatia wakulima tayari wameshaziokota korosho zao na kuziweka majumbani mwao," alisema Makere.

Makere aliwaomba wakulima kuwa wavumilivu wakati uongozi wa chama hicho ukiendelea kutatua changamoto za upatikanaji wa vifungashio ambavyo tayari vimeanza kuwasili nchini kwetu.

Said Ally, Mwajuma Selemani na Ahamadi Mburugenda ni wakulima kutoka vijiji vya Mnali na Kitunda Lindi, ambao wamepeleka korosho zao Chama cha Msingi cha (KITUMIKI AMCOS) wameonyesha hofu kufuatia bei zitakazotumika kununuliwa na wafanyabiashara watakaojitokeza kuzinunua.

Walisema gharama za uendeshaji mashamba ya korosho ni kubwa hivyo ni vyema serikali ikatoa bei elekezi ili wakulima waweze kutambua kabla ya kupeleka zao hilo kwenye vyama vikuu vya ushirika.

Mnada wa kwanza kwa Chama cha Lindi Mwambao unatarajia kufanyika Oktoba 10 mwaka huu, badala ya Oktoba 03, mwaka huu.

# Mamia wanakijiji watibiwa macho bure

**Na Futuna Seleman,** RUFIJI

ZAIDI ya wakazi 300 wa kijiji cha Nyaminywiri wamepatiwa matibabu ya macho, 23 wakifanyiwa upasuaji bure wakiwamo wenye matatizo ya mtoto wa jicho katika Kituo cha Afya Nyaminywiri Rufiji mkoani Pwani.

Rais wa Lions Club, Mzizima Hitesh Solank, akizungumzia kampeni ya siku mbili kupiga kambi kituoni hapo wakishirikiana na timu ya madaktari kutoka Dar es Salaam na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, alisema wamekuwa wakitoa huduma hiyo katika mikoa tofauti nchini licha ya kusimama kwa muda kutokana na ugonjwa wa corona.

"Katika kambi licha ya kutoa huduma za matibabu ya macho na wenye matatizo kupewa miwani, pia kwa wagonjwa tunatoa huduma ya maji na chakula kwa waliopatiwa huduma hiyo," alisema Pandesh.

Aidha, alisema mkakati wao ni kufika katika mikoa tofauti nchini kutokana na tatizo la macho kuwasumbua wananchi wengi.

"Tumeanza Mwanza, Morogoro na Tanga. Kwa mwaka tunapiga kambi tatu inategemea mahitaji ya wagonjwa na wafadhili, kwa kawaida kambi moja tunapokea wagonjwa 2,000 hadi 3,000 na tunapata watu wengi... matatizo ya macho yanahitaji upasuaji na tunawapatia huduma hiyo," alisema.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Dk. Ali Mbikilwa, alisema wadau wa maendeleo Lions Club Mzizima kwa kushirikiana na wasimamizi wa afya mkoa wa Pwani, timu ya madaktari wa afya Dar es Salaam na wilaya yake wamefanya kazi hiyo kusaidia wananchi wenye uhitaji.

"Huduma hizi za siku mbili zimeibua wananchi wengi kuja kutibiwa bure kituoni hapa...na hii inaonyesha wananchi wana uelewa mkubwa juu ya umuhimu wa kutafuta suluhisho la matatizo ya afya yanayowakabili," alisema Dk. Ali.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF, klabu, wachezaji ilindeni mikataba yenu

**WAKATI** Ligi Kuu Tanzania Bara ndio kwanza imeanza kushika kasi, sakata la mchezaji wa kimataifa wa Simba kutoka Ghana, Bernard Morrison, limerejea katika sura nyingine.

Awali Morrison aliyetua nchini mapema Januari, mwaka huu na kusajiliwa na Yanga, aliwasilisha malalamiko katika Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), akilalamika kutotambua mkataba mpya na klabu hiyo.

Morrison aliweka wazi kwamba mkataba aliokuwa anautambua ni ule uliokuwa unamalizika Julai mwaka huu, na nyota huyo aliukana mkataba mpya ambao ulielezwa utamalizika Julai mwakani.

Winga huyo alishinda kesi yake iliyokuwa inasikilizwa na Kamati ya Hadhi na Sheria ya TFF, inayoongozwa na mwenyekiti wake, Elias Mwanjala.

Mchezaji huyo alitangazwa kuwa huru na aliruhusiwa kujiunga na klabu yoyote, na siku chache alitangazwa kujiunga na watani zao na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba.

Wiki iliyopita, Yanga imeibuka na malalamiko kwamba mkataba wa Simba na Morrison ni batili kwa sababu umebainika kuwa na mapungufu. Ikumbukwe muda wa kuwasilisha malalamiko ulishapita na anayelalamika sasa ni mhusika wa pande yoyote kwenye mkataba huo.

Hata hivyo, kwa busara za TFF, imepokea malalamiko hayo na kamati husika imepanga kukutana Oktoba 12, ili kuyapitia na hatimaye kutoa hukumu.

Filamu hizi zitazotokea na kujirudia kila msimu, zinatufundisha kuwa kuna mapungufu katika zoezi zima la mchakato wa kusajili wachezaji kwa ajili ya kushiriki Ligi Kuu Bara, Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili, Ligi Kuu ya Wanawake na mashindano ya Kombe la FA.

Kama hii haitoshi, inaonekana wachezaji wengi wanapewa leseni hali ya kuwa usajili wao haujakamilika.

Kwa kuendelea kuziruhusu klabu kutumia wachezaji ambao usajili wao umezungukwa na 'ujanja ujanja', hupelekea wawakilishi wetu kwenye mashindano ya kimataifa kukwama kutumia baadhi ya nyota iliyokuwa nayo.

Nipashe tunashangaa kuona TFF inaitisha kikao kujadili uhalali wa mkataba wa Morrison, wakati yenyewe ilishatoa tamko kuwa klabu ambayo haitawasilisha mikataba ya wachezaji wake, basi timu husika haitapatiwa leseni ya kumtumia.

Tunaamini TFF ilifuata taratibu hizo na kutoa leseni kwa Morrison ili aitumikie klabu yake mpya ya Simba na kama shirikisho hilo lilikiuka taratibu ilizojiwekea yenyewe, inamaana mchakato mzima wa usajili huenda umegubikwa na sintofahamu nyingi zaidi.

Leo unazungumziwa mkataba wa Morrison wa Simba, lakini huenda wachezaji wengine wasiokuwa na majina makubwa pia wamepewa leseni au wamepitishwa kuzitumikia timu bila ya taratibu za uhamishi kufuatwa kikamilifu.

Umefika wakati wa TFF, klabu na wachezaji kufanya majukumu yao kisasa na kwa weledi ili kuruhusu masuala mengine ya maendeleo kufanyika badala ya sasa kutumia nguvu kubwa kuangalia 'adui' yako alikosea wapi ili aadhibiwe.

Mbali na klabu kuwa makini, TFF pia inatakiwa kuwachukulia hatua wadau wote ambao wamekuwa wakisambaza nyaraka za shirikisho hilo, jambo ambalo linawapunguzia heshima kwenye tasnia hii ya michezo.

Kama inawezekana mikataba ya wachezaji wa soka inawekwa hadharani, siku moja pia wadau watashuhudia wakiona siri nyingine za taasisi hiyo zikiwa nje na huenda zikahatarisha usalama wa mambo mbalimbali.

Maendeleo ya soka hayapatikani kwa kuonyesha kiwango bora uwanjani, lakini pia kwa kufuata taratibu, kanuni na sheria zilizowekwa bila ya upendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Meneja Mkwakwani ni mfano wa kuigwa

Na Adam Fungamwangwo

**NILIKUWA** naangalia mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Coastal Union dhidi ya JKT Tanzania. Ilikuwa Septemba 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini, Tanga.

Kwanza kabisa nilijua mechi hiyo inachezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam, Uhuru au Azam Complex.

Lakini akili ikanijia kuwa Coastal Union inacheza na JKT Tanzania ambayo Makao Makuu yao yako jijini, Dodoma, hivyo timu kutoka Tanga na Dodoma haziwezi kucheza Dar es Salaam.

Hadi akili yangu ilipokubali kuwa uwanja ule wa nyumbani wa Coastal Union ni Mkwakwani na ilichukua dakika nyingi kidogo.

Nikikumbuka msimu uliopita jinsi uwanja ulivyokuwa na sasa ulivyo ni vitu viwili tofauti.

Niliona mechi kadhaa zilizochezwa kwenye uwanja huo misimu miwili iliyopita, ulikuwa ni moja kati ya viwanja vibovu mno ndani na nje ya uwanja.

Sehemu ya kuchezea ilikuwa na udongo uliochanganyikana na mchanga zaidi kuliko nyasi. Wakati wachezaji wakipambana uwanjani, vumbi lilitimka na kuondoa ladha halisi ya mchezo wa soka.

Wachezaji ilibidi watumie mbinu za ziada, ukiacha zile za kawaida za ufundi wa mpira uwanjani.

Mpira unaweza kudunda na kubadilisha uelekeo, kuna wakati unaweza kwenda kasi zaidi au taratibu zaidi kuliko mchezaji alivyotaka uwe.

Kwa sasa haiko hivyo. Uwanja wa Mkwakwani umekuwa ni mmoja wa viwanja vilivyoboreshwa kwenye sehemu ya kuchezea. Una majani ya kijani ambayo yanavutia hata kutazama kwenye televisheni na hata wachezaji hawapati tabu kupiga pasi na hata kucheza kwenye mifumo inayotakiwa.

Nitoe pongezi za kwanza kwa meneja wa Uwanja wa Mkwakwani kwa kuubadilisha kabisa uwanja huo ambao ulikuwa hautamaniki hapo kabla.

Pongezi za pili ziende kwa Chama cha Soka cha Mkoa wa Tanga (TRFA), kwa kuungana na wamiliki wa uwanja huo kuhakikisha wanautengeneza uwanja huo ili timu yao pekee inayocheza Ligi Kuu ya Coastal Union ishiriki kwa ukamilifu.

Lakini pongezi zingine nizipeleke kwa viongozi wa Coastal Union kwa kushirikiana na uongozi wa mkoa Tanga na uongozi wa uwanja kuhakikisha uwanja huo unakarabatiwa na kuwa wa kuridhisha.

Nadhani wasimamizi wa viwanja vyote wangekuwa na mawazo kama ya wenzao wa Mkwakwani, viwanja vingi nchini vingekuwa bora.

Hivi karibuni Bodi ya Ligi ilivifungia viwanja vya Gwambina ulioko Mwanza, Karume (Mara), Jamhuri Morogoro, Ushirika (Moshi) na Uwanja wa Mlandizi mkoani Pwani.

Ukiangalia mapungufu yaliyotolewa ni sehemu za kuchezea, pamoja na vyumba vya kubadilishia nguo.

Hata hivyo, matatizo makubwa sana kwenye viwanja vya Tanzania ni sehemu za kuchezea.

Viwanja vingi majani yake ni ya kubahatisha. Yamekauka na uwanja kuwa mkavu kama shamba wakati wa kiangazi.

Na kuna baadhi ya viwanja pia vina nyasi, lakini bado uwanja ni mgumu mno, hivyo mpira unadundadunda na kuwachanganya wachezaji.

Kinachofurahisha kwa Uwanja wa Mkwakwani ni kuwa pamoja na nyasi zake kuwa za kijani kama Uwanja wa Taifa, lakini pia ardhi yake inaonekana imemwagiwa maji kwa muda mrefu, hivyo mpira unatambaa tu kwenye nyasi.

Inaeleweka kuwa Tanga ni mkoa ulio ukanda wa Pwani ambako muda mrefu kunakuwa na jua kali na joto pia, lakini wameweza kuufanya uwanja kuwa bora, lakini kuna mikoa kama Morogoro na Kilimanjaro, hii miezi mingi inakuwa na baridi, lakini cha ajabu inashindwa hata kutengeneza uwanja ukawa na nyasi za kuvutia na udongo usiokuwa mkavu.

Kwa sababu viwanja vingi Tanzania ni mali ya Chama cha Mapinduzi (CCM), nadhani inafaa sasa mameneja wa viwanja vingine kuwasiliana na meneja wa Uwanja wa CCM Mkwakwani au hata CCM Kirumba kuwauliza ni mbinu gani wanazotumia na kuvifanya viwanja hivyo kuwa bora zaidi, ili na wao wachukue mbinu hizo wazihamishie kwenye viwanja vyao.

Meneja wa Mkwakwani anaweza kabisa kuwaambia mbinu au jinsi gani alivyoutoa uwanja huo kutoka kuwa mbovu na kuwa bora zaidi kwa viwanja vya mikoani kwa sasa nchini Tanzania.

# Wanafunzi 400 wasoma kwa kupokezana Msalala

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ZAIDI ya wanafunzi 400 wa darasa la kwanza Shule ya Msingi Bugarama, Halmashauri ya Msalala, wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wanalazimika kusoma kwa awamu kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Hali hiyo imeelezwa kusababisha usumbufu kwa walimu na wanafunzi kutofikia lengo la kukamilisha mitaala ya kujifunzia na kufundishia masomo mbalimbali kwa muda uliopangwa.

Shule hiyo ina vyumba vya madarasa 18, vinavyoendelea kujengwa ni vine, huku idadi ya wanafunzi katika shule hiyo ikiwa ni 2,324, wasichana 1,187 na wavulana 1,137, huku mahitaji ya vyumba vipya vya madarasa ikiwa ni 32.

Mkuu wa shule hiyo Mwalimu, Kubebeka Leonard, alisema hayo wakati wa hafla maalumu ya wadau wa sekta ya elimu waliofika katika shule hiyo kutoa msaada wa saruji mifuko 200 kwa ajili ya kujenga vyumba vya madarasa katika shule hiyo, ili kuondoa tatizo hilo.

Alisema baada ya kuanza utekelezaji wa sera ya elimu bure, wananchi wa maeneo hayo ambayo yanazungukwa na migodi midogo walihamasika kupeleleka watoto wao shule, na kwamba kwa mwaka 2020 wanafunzi walioandikishwa kuanza darasa la kwanza pekee walikuwa ni 400.

Alisema kutokana na uwapo wa tatizo hilo kwa sasa wanafunzi wa darasa la kwanza wanalazimika kusoma kwa awamu mbili asubuhi na jioni na kila awamu ina wanafunzi zaidi ya 150 kwa darasa moja.

Darasa la kwanza lina mikondo minne ili kuwawezesha kujifunza vizuri.“Tuliitisha harambee ya kuchagia ujenzi wa madarasa shuleni, tuliwaita wadau mbalimbali ukiwamo mgodi wa Barrick Bulyankulu ambao walitusaidia kupata fedha zaidi ya Sh. milioni 100 ambazo zimeanza kujenga vyumba vinne vya madarasa ili kupunguza tatizo hili ambalo linaikabili shule yetu,” alisema Leornad.

Akipokea saruji hiyo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala, Ofisa Elimu Msingi, Cosmas Magigi, aliwapongeza wadau hao wa elimu ambao ni Kampuni ya Ako Group Limited kwa kutoa msaada huo utakaosaidia kutatua changamoto ya uhaba wa vyumba vya madarasa katika shule hiyo.

Alisema idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa kuanza darasa la kwanza kila mwaka katika halmashauri hiyo, inakadiriwa kufikia 8,000 hali ambayo inasababisha uhaba wa vyumba vya madarasa na kuwataka wadau na jamii kujitokeza kuchangia kwa hiari katika ujenzi wa vyumba vya madarasa, ili kuwasaidia walimu kufundisha vizuri.

Alisema kuwa kwa mujibu wa sera ya elimu, mwalimu anatakiwa kufundisha wanafunzi 45 kwa darasa moja pekee, lakini kwa shule hiyo ni vigumu kutokana na uhaba wa vyumba na kwamba wanalazimika kufundisha wanafunzi zaidi ya 150 kwa darasa moja.

Kwa upande wake, Meneja wa Kampuni ya Ako Group Limited, Atanasi Kahigi, alisema wataendelea kushirikiana na jamii kutatua changamoto mbalimbali za elimu na wametoa saruji mifuko 200 zilizogharimu Sh. milioni nne.



Bwanashamba wa Shirika la World Vegetables Center la Tengeru, wilayani Arumeru, mkoani Arusha, Omary Mbwambo (kulia), akionyesha namna ya kupika udongo kwa ajili ya kuua magugu na wadudu kabla ya kuotesha mbegu kwa waandishi wa habari, walipotembelea shirika hilo mwishoni mwa wiki. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wakulima korosho watahadharishwa

**Na Ashton Balaigwa,** DODOMA

WAKULIMA wa korosho nchini wametahadharishwa kuwa endapo hawatakabiliana na visumbufu vya zao hilo ikiwamo magonjwa na wadudu waharibifu, watapata hasara kati ya asilimia 60 hadi 100.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Mtafiti wa visumbufu vya mazao kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kituo cha Naliendele cha mkoani Mtwara, Dk. Wilson Nene, alipokuwa akitoa mafunzo ya kilimo bora cha korosho kwa wakulima wapya wa zao hilo wilayani Chemba, mkoani Dodoma.

Alisema korosho inakabiliwa na magonjwa na uwapo wa wadudu waharibifu wakiwamo mbu wa mikorosho na mbu wa minazi ambao wanashambulia mimea ya mikorosho na kusababisha isitoe matunda na hivyo mkulima kupata hasara.

“Mikorosho isipotunzwa kwa mkulima kupambana na visumbufu vyake kama vile magonjwa na wadudu, mkulima anaweza kupata hasara ya kati ya asilimia 60 na 100, hapa namaanisha anaweza kupata mazao machache au kukosa kabisa,” alisema Dk. Nene.

Alisema kuwa ili kuwasaidia wakulima kupambana na visumbufu hivyo, TARI Kituo cha Naliendele imeshafanya utafiti na kubaini njia tatu za kukabiliana na visumbufu hivyo vya mikorosho.

Dk. Nene alizitaja njia hizo kuwa ni ya asili, kutengeneza mazingira ambayo sio rafiki kwa vimelea au wadudu na kutumia viuatilifu ambavyo vimeonyesha kama vitatumika kwa utaratibu mzuri na kufuata masharti vinasaidia kutokomeza visumbufu hivyo.

Alisema njia hizo tatu zikitumika kwa pamoja, mkulima anaweza kudhibiti kabisa visumbufu vya zao la korosho na hatimaye akavuna mazao mengi na kujiingizia kipato cha kutosha.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Saimon Odunga, alisema katika maeneo mapya ambayo yameanza kulima zao la korosho, wakulima wanahitaji elimu ya kutosha kuanzia kuandaa shamba, kupanda miche ya mikorosho, kutunza mashamba na kuvuna.

Chacha alisema kuwa ili wakulima wahamasike kulima korosho, ni wajibu wa viongozi wa serikali kuwatembelea na kuwapatia elimu ya mara kwa mara kwa lengo la kuwawezesha kulima kwa tija.

Alishukuru TARI pamoja na Bodi ya Korosho kwa kufika wilayani Chemba kutoa elimu ya kilimo bora cha korosho kwa maelezo kuwa hatua hiyo itasaidia wakulima wa wilaya hiyo kulima korosho kwa wingi na kwa tija.

Kwa upande wake, Mratibu wa korosho nchini, Dk. Geradina Mzena, alisema kuwa lengo la TARI kupitia Kituo cha Naliendele ni kutoa elimu ya kilimo bora cha korosho kwa wakulima wote ndani ya mikoa 17 inayolima zao hilo nchini.

Dk. Mzena alisema kuwa elimu hiyo wataitoa kwa baadhi ya wakulima pamoja na maofisa ugani ambao ndio watakwenda kuwaelimisha wakulima wengine kwenye maeneo yao.

# Watendaji ardhi wakumbushwa kushirikiana

**Na Christina Mwakangale**

WATENDAJI wa Sekta ya Ardhi katika Halmashauri ya Manyoni mkoani Singida, wametakiwa kufanya kazi kwa ushirikiano ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yao.

Kaimu Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa huo, Speratus Ruteganya, aliyasema hayo kwenye kampeni maalum iliyozinduliwa na Wizara ya Ardhi siku ya elimu ya mlipakodi ambayo hutekelezwa kila Ijumaa.

Akizungumza na kikosi kazi maalum kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kilichofika wilayani Manyoni kutoa elimu kwa umma kuhusu kodi, Ruteganya alisema umoja na ushirikiano ili kufikia malengo katika sekta hiyo lazima kuwapo ushirikiano.

“Wananchi wanachohitaji ni elimu tu kwani wakielimika kodi itapatikana pamoja na taarifa muhimu za umiliki,” alisema Ruteganya.

Kiongozi wa kikosi kazi kutoka wizara hiyo, Adam Komba, alisema, lengo la wizara kuanzisha siku ya elimu kwa mlipakodi ni kuhakikisha wananchi wanapewa elimu kuhusu umuhimu wa kulipa kodi pamoja na kuboresha taarifa zao za umiliki.

Alisisitiza kwamba, kutokana na mabadiliko ya teknolojia hasa kwenye utoaji wa huduma, wizara ina mpango wa kuboresha mifumo yake ya utoaji huduma.

Ofisa Ardhi mteule wa wilaya hiyo, Zamzam Seif, aliishukuru wizara kwa hatua iliyochukua ya kuboresha taarifa za wamiliki.

Alisema kitendo cha wizara kutuma kikosi kazi wilayani kimewapa moyo na nguvu mpya ya kufanya kazi.

Siku ya Elimu ya Mlipakodi ni kampeni maalum iliyoanzishwa na wizara hiyo kila Ijumaa kwa kupita mitaani kutoa elimu nyumba kwa nyumba, ili kuhakikisha wamiliki wanajua sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayoisimamia sekta hiyo.

## Mgombea ACT aeleza sababu za kugombea

**Na Said Hamdani,** LINDI

MGOMBEA udiwani Kata ya Msinjahili, Jimbo la Lindi Mjini kwa tiketi ya ACT-Wazalendo, Abdallah Faustine Khalfani, amesema uzalendo alionao kutaka kuwatumikia wananchi ndicho kilichomsukuma kugombea nafasi hiyo mwaka huu.

Khalfani ameyaeleza hayo alipokuwa anaomba ridhaa ya kupewa dhamana hiyo kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika Mtaa wa Msonobarini mjini hapa.

Akiomba ridhaa hiyo, alisema uthubutu na uzalendo alionao wa kupenda kwao ndicho kilichomsukuma ajitose kuwania nafasi hiyo ya uongozi ili aweze kushirikiana na wananchi kujiletea maendeleo ya kweli na kurejesha heshima ya mji wa Lindi.

Alisema kufuatia ugumu wa maisha unaochangiwa na mkoa kutokuwa na vitega uchumi, vikiwamo viwanda kumewafanya vijana wazawa kukimbilia maeneo mengine kutafuta unafuu wa maisha. Khalfani alisema Kata ya Msinjahili licha ya ukubwa wa eneo lake, haina zahanati, hali inayowalazimu wananchi wanapokabiliwa na tatizo la kuugua kufuata huduma za matibabu kata jirani za Nachingwea, Zahanati ya Jeshi la Magereza, Makonde na Hospitali ya Mkoa ya Sokoine.

Alisema uongozi wa kata umeshindwa kuishawishi Halmashauri ya Manispaa kujenga zahanati ili kuwapunguzia wananchi tatizo la kukosa huduma za tiba, licha ya kuwa na maeneo mengi ya wazi. Mgombea huyo aliwaeleza wananchi wa Kata ya Msinjahili kuwa iwapo watamchagua kuwa diwani wao atahakikisha inakuwa na zahanati ili kuwapunguzia tatizo la kutembea mwendo mrefu kufuata tiba maeneo mengine. "Ndugu zangu, wazee na mabibi zangu mkinipa ridhaa ya kuwa diwani wenu, nakuhakikishieni zahanati inapatikana ndani ya kata yetu," alisema Khalfani. Bakari Fundi, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa ACT-Wazalendo Jimbo la Lindi Mjini, aliwaambia wananchi kutofanya makosa kuwachagua tena wagombea wanaotokana na CCM kwa kile alichokielezea wamekosa mwelekeo katika kuijenga Manispaa na Mkoa kwa ujumla.

Fundi alisema kabla na baada ya Taifa kupata uhuru, mkoa ulikuwa na neema nyingi, ikiwamo viwanda ambavyo vilitumika kujipatia ajira, jambo ambalo kwa sasa ni tofauti.



Ofisa Elimu Mkoa wa Pwani, Abdul Maulid, akimkabidhi cheti mmoja wa wahitimu wa kidato cha nne Shule ya St. Anne Marie Academy, wakati wa mahafali shuleni hapo, Mbezi kwa Msuguri, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Plan International yatoa pikipiki 18 kupunguza vifo

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Plan International limetoa msaada wa pikipiki 18 zenye thamani ya Sh. milioni 43, kusaidia serikali katika mpango wa huduma mkoba unaotoa chanjo itakayopunguza vifo vya wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika Halmashauri ya Mlimba, wilayani Kilombero.

Kaimu Meneja wa Shirika hilo programu ya Ifakara, Silvin Masele, alisema kuwa lengo la kutoa pikipiki hizo ni kutafuta ufumbuzi wa kukabiliana na changamoto ya miundombinu ambayo inakwamisha juhudi za kufikisha huduma hiyo kwa wananchi.

Alisema changamoto ya miundombinu ilikuwa ikisababisha watumishi kushindwa kuwafikia wananchi kwa wakati hasa wajawazito katika maeneo ambayo gari maalumu lililokuwa linatoa huduma ya chanjo kushindwa kufika.

"Huduma mkoba imelenga kutoa upimaji wa mimba na afya kwa wajawazito, kutoa chanjo za magonjwa na ushauri kuhusu lishe na elimu hasa kwa watu wanaoishi vijijini, lakini changamoto ilikuwa ni gari kushindwa kufika ndio maana sisi tukaona tuongeze nguvu kwa serikali kwa kutoa hizi pikipiki 18, ili watumishi wa afya wawafikie wananchi kwa wakati," alisema Masele.

Abdulkadri Amir ni Mratibu wa chanjo mkoa wa Morogoro, alilishukuru Shirika la Plan International kwa ushirikiano wa karibu na serikali ya Wilaya ya Kilombero kwa muda mrefu katika nyanja mbalimbali zikiwamo huduma za afya, haki za watoto, elimu, utunzaji wa mazingira.

Alisema kuwa msaada huo waliopokea mwendelezo wa awamu ya kwanza wa mpango wa huduma mkoba inayoendelea kutolewa wilayani humo kwa kutumia gari maalum (mobile van), Shirika hilo ndio lililotoa gari maalum la wagonjwa ili kuwafikia walengwa.

"Tutegemea kuwa pikipiki hizi zitaenda kufanikisha mpango huu kwa kiasi kikubwa sana kwa sababu kwa kutumia gari maalum tulifikia vijiji 26 pekee kati ya 62 vilivyopo hapa mlimba, lakini sasa tutaweza kuvifikia vyote," alisema Abdulkadri.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha miaka minne tangu 2016 hadi 2019 mradi huo ulifikia kata 12 kati ya kata 16 sawa na asilimia 75, huku vituo mkoba 44 kati ya 61 sawa na asilimia 72 vimenufaika na mpango huo.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mlimba, Faraja Nakoa, aliwataka wahudumu wote wa afya wanaotekeleza mradi huo ambao ndio waliokabidhiwa pikipiki hizo kwenda kuzitumia katika kazi iliyokusudiwa.

# JPM apongezwa kuamini wazalendo kwenye miradi

**Na Veronica Simba,** RUFIJI

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Leonard Masanja, amempongeza Rais John Magufuli kwa kuwaamini wazalendo katika kusimamia utekelezwaji wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP).

Alitoa pongezi hizo juzi wakati akizungumza na wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REB), waliotembelea mradi huo unaotekelezwa wilayani Rufiji, Mkoa wa Pwani, ili kujionea maendeleo yake.

Masanja alisema kuwa hatua ya rais kuwaamini wataalamu wazalendo kusimamia usanifu wa awali, ununuzi na hata usimamizi wa utekelezaji wa mradi wenyewe, bila kushirikisha wataalamu wa kigeni ni ushahidi kuwa Tanzania ina hazina ya wataalamu mahiri.

"Kupitia mradi huu, tumeudhihirishia ulimwengu kuwa Tanzania ina wataalamu mahiri na kwamba sisi wenyewe tunaweza kusimamia miradi yetu."

Akifafanua, alisema serikali iliamua kuwatumia wataalamu kutoka TANROADS (TANROADS Engineering Consulting Unit - TECU), kama Mshauri Mwelekezi wa Mradi na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), wakiwa wawakilishi wa serikali katika kusimamia mradi husika ili kuhakikisha mkandarasi anatekeleza kazi zote kwa mujibu wa mkataba.

Alisema, jambo la kujivunia zaidi ni kuwa mradi huo unatekelezwa na fedha za serikali kwa asilimia 100, hivyo akawataka Watanzania kujivunia mradi huo kwa kuwa nchi inaumiliki kikamilifu.

Awali, akitoa wasilisho la mradi kwa ujumbe husika, Mhandisi Mkazi wa mradi huo, Mushubila Kamuhabwa, alisema katika hatua ya ujenzi inayoendelea sasa, mradi umewezesha uzalendo na mshikamano wa hali ya juu kwa vijana wa kitanzania wanaofanya kazi za ujenzi.

"Ni kama wakati ule vijana walipokuwa wakishiriki mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa. Utawakuta vijana hawa wakiimba nyimbo za kizalendo wakati wanafanya kazi na pia wakishirikiana kwa kila jambo, hali inayoonyesha wazi wanajisikia fahari kuwa sehemu ya utekelezaji wa mradi huu."

Vilevile, Mhandisi Kamuhabwa alisema miongoni mwa waajiriwa 5,500 wa mradi waliopo sasa, Watanzania ni 4,900 ambao ni asilimia 90 ya waajiriwa wote, jambo ambalo linadhihirisha dhamira ya serikali kuhakikisha Watanzania wanapewa kipaumbele katika kila sekta ya mradi huo.

Naye Kaimu Kamishna wa umeme na Nishati Jadidifu kutoka Wizara ya Nishati, Edward Ishengoma, alisema kuwa wizara iliona umuhimu wa kuandaa ziara hiyo kwa ajili ya wajumbe wa menejimenti yake, ili kuwawezesha kujionea kwa macho kinachofanyika ikizingatiwa kuwa ndiyo wizara mama inayohusika na mradi huo.

HABARI KITAIFA

# Bosi TAKUKURU: Vita dhidi ya rushwa imepunguza umaskini

**Na Hamisi Nasri, MASASI**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) imesema kazi ya mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi nchini iliyofanywa na serikali ya awamu ya tano inaonyesha kuwa hali ya umaskini Tanzania imepungua kutoka asilimia 34.4 hadi kufikia asilimia 26.8.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki wilayani Masasi mkoani Mtwara na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbungo, alipokuwa akizungumza na wakuu wa taasisi mbalimbali za serikali, taasisi zisizo za kiserikali na wananchi kwenye uzinduzi wa jengo jipya la ofisi ya Wilaya ya Masasi lililojengwa kwa kutumia fedha za serikali.

Jenerali Mbungo alisema ripoti ya Benki ya Dunia Septemba 26, mwaka 2019 imeeleza kuwa Tanzania imeongoza kwa kupunguza hali ya kiwango cha umaskini miongoni mwa nchi za Afrika zilizoko kusini mwa Jangwa la Sahara.

Alieleza ripoti nyingine ya Benki ya Dunia ya Human Capital' The Real Wealth of Nations, iliyotoka Julai, 2019 ilionyesha kuwa umaskini Tanzania umepungua kutoka asilimia 34.4 hadi asilimia 26.8 na hiyo imetokana na kazi kubwa ya mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa na ufisadi iliyofanywa na serikali ya awamu ya tano chini ya Rais. John Magufuli.

Mkurugenzi huo alisema ufanisi na jitihada za serikali katika mapambano dhidi ya rushwa nchini kwa mwaka 2018/19 zimeendelea kuonekana pia kupitia taarifa za utafiti wa kupima hali ya rushwa duniani unaofanywa na wadau wa mapambano dhidi ya rushwa na utawala bora kama Taasisi za Transparency International (TI), MO Ibrahim na Afro barometer.

Alisema kuwa taarifa za taasisi hizo zote zinaonyesha kuwa kwa miaka mitatu mfululizo tangu mwaka 2016 hadi 2018, Tanzania imeendelea kufanya vyema katika mapambano dhidi ya rushwa na utawala bora.

"Mafanikio haya na mengine mengi yanaadhimisha hatua kubwa ambayo imefanywa na serikali katika kuhakikisha kuwa kero ya rushwa na ufisadi nchini inadhibitiwa katika taifa letu, lakini wananchi pia wameshiriki katika kutoa ushirikiano kwa serikali yao...sisi TAKUKURU tutaendelea kuwa wakali kwa wala rushwa," alisema Jenerali Mbungo.



Wachuuzi wa machungwa wakisubiri wateja katika Soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. Chungwa moja linauzwa 130/-, kwa bei ya jumla. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Utafiti wa kasi magonjwa yasiyoambukiza watakiwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KATIBU Tawala Mkoa wa Pwani, Dk. Delphine Magere, ametoa wito kwa wahitimu wa kada ya afya kufanya utafiti ni kwa namna gani wanaweza kusaidia jamii kutafuta suluhisho la magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo kisukari na shinikizo la damu.

Dk. Magere alitoa wito huo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya 52 ya Chuo cha Afya na Sayansi kilichopo Tumbi Mjini Kibaha.

Alisema kumekuwa na ongezeko la wagonjwa wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama shinikizo la damu na kisukari.

"Nafahamu hali yetu ya maisha inachangia sana kuongezeka kwa maradhi haya, lakini kuona namna ya kuisaidia jamii yetu ambayo inataabika kwa kuwapo kwa Ukimwi, pia magonjwa yasiyoambukiza," alisema.

Aliwataka pia wahitimu kuwa na mikakati ya kujiendeleza badala ya kuridhika na hatua waliyofikia ili kufikia ndoto za mafanikio.

Akizungumzia kuhusiana na namna ya kutatua changamoto za chuo hicho, alisema, atatatumia nafasi yake kuwakutanisha wadau wa viwanda na biashara pamoja na uongozi wa Shirika la Elimu Kibaha na taasisi zake ili kwa pamoja waweze kujadili na kukubaliana namna ya kuimarisha miundombinu katika chuo na taasisi nyingine za shirika.

Akiwa katika mahafali hayo, aliendesha harambee na kukusanya Sh. milioni 6.6, ahadi Sh. milioni 5.6 fedha taslimu ikiwa ni Sh. 365,000, ambapo alipongeza shirika hilo kwa kuwa na mipango endelevu kwa maslahi ya Watanzania.

Mkuu wa chuo hicho, Dk. Gissenge Lija, alisema, tangu chuo hicho kianzishwe mwaka 1968, wahitimu zaidi ya 2,000 wamehitimu katika chuo hicho katika fani za waganga wasaidizi vijijini, Shahada ya Utabibu, Stahada ya Uuguzi na ukunga na kozi ya wahudumu wa afya ya jamii katika ngazi ya cheti.

Dk. Lija alisema, chuo hicho kwa sasa kina uwezo wa kupokea wanachuo 160 kwa madarasa mawili yaliyopo pamoja na kupokea naombi zaidi ya 5,000 wenye sifa kwenye udahili unaosimamiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE).

Alisema kwa sasa chuo hicho kinakabiliwa na changamoto ya uhaba wa miundombinu inatosababisha kushindwa kuanzishwa kwa kozi mpya za stashahada ya famasia na maabara ya uchunguzi ambazo tayari zimeruhusiwa na Baraza la Taifa la Elimu la Ufundi (NACTE).

# Kiswaga aahidi kupeleka huduma bora afya Magu

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MGOMBEA ubunge Jimbo la Magu kwa tiketi ya CCM, Boniventura Destery Kiswaga, ameahidi kuwa atakamilisha ujenzi wa zahanati 10, ili kusogeza huduma ya afya kwa wananchi hasa kinamama na watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Aliyasema hayo wakati akiwa katika mkutano wa kampeni kijiji cha Lutale Kata ya Lutale, na kwamba ataendelea kusogeza zaidi huduma za afya kila kijiji ili kuwezesha kuokoa zaidi maisha ya mama wajawazito na watoto.

"Kwa sasa hapa Lutale mama anatembea umbali mrefu kwenda kijiji kingine kuhudhuria kliniki kupata huduma mbalimbali ikiwamo afya ya uzazi, nichagueni tukamilishe zahanati yenu tuliyoanzisha," alisema.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita amejitahidi kuboresha huduma za afya kwa kuishawishi serikali na wadau wa maendeleo kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha na kupanua vituo vitatu vya afya, vya Kahangara HC, Lugeye HC na Kabila HC.

Anasema serikali imetoa fedha za kujenga jengo la kisasa la wagonjwa wa nje (OPD) katika Hospitali ya Wilaya ya Magu, amewezesha ununuzi wa vifaa tiba X-ray mashine na Utral sound ambazo huduma hizo hapo awali walikuwa wakipata katika hospitali teule ya mkoa ya Sekoutoure na Bugando.

"Nawahakikishia kuwa pamoja na kuchangia ujenzi wa zahanati tisa ambazo maboma yamekamilika nakusudia kuzikamilisha mapema iwezekanavyo katika awamu ijayo nikishachaguliwa.

# 5,000 waishukuru serikali kwa ufadhili wa masomo

**Na Yasmine Ptotace**

WANAFUNZI zaidi ya 5,000 wakiofadhiliwa na serikali kusoma kupitia vyuo vya ufundi wamehitimu mafunzo yao na kuishukuru serikali.

Shukrani hizo zilitolewa na wanafunzi hao katika mahafali yao yaliyofanyika Don Bosco, jijini Dar es Salaam.

Ashura Juma, mhitimu katika fani ya ushonaji, alisema kama asingepatiwa mafunzo hayo, asingejua kushona.

"Baada ya kupatiwa mafunzo nimeweza kujua kushona na nikitoka hapa chuo najiajiri mwenyewe," alisema.

Melchades Nshamba, Mtendaji Don Bosco Networks Tanzania, aliipongeza serikali ya kwa kuanzisha mradi kwa ajili ya kuwezesha vijana kupata elimu ya ujasiriamali na kwamba mradi huo utakuwa ni mkombozi kwa wahitimu.

"Mradi wa mafunzo ya muda mfupi ulifadhiliwa chini ya serikali ya awamu ya tano ya Rais John Magufuli, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi , Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)," alisema.

Alisema ufadhili huo kwa vijana ulihusisha gharama za mafunzo kwa asilimia 100.

Alisema vijana walipatiwa nauli ya Sh. 100,000 kwa miezi sita ya mafunzo yao.

Alisema vijana hao walipatikana kwa njia ya udahili katika vituo 18 vya mafunzo ya ufundi vilivyopo katika baadhi ya mikoa.

Alisema vijana zaidi ya 9,000 waliomba, lakini waliokidhi vigezo na kuchaguliwa ni 5,847 katika fani 18.

# Asilimia 67 waliopima Dar wana uzito wa kupindukia

**Na Christina Mwakangale**

WATU 4,461 kati ya 6,691 walibainika kuwa na uzito uliopindukia jijini Dar es Salaam.

Watu hao wana uzito mkubwa na kuwa katika hatari ya kupata magonjwa yasiyo yakuambukiza ikiwamo magonjwa ya moyo na kisukari.

Hali hiyo inatajwa kutokana na lishe duni na kutofanya mazoezi maeneo ya mijini ikiwamo, Dar es Salaam.

Bingwa wa Magonjwa ya Moyo na Mkuu wa Idara ya Utafiti na Mafunzo katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Pedro Pallangyo, alibainisha hayo alipozungumza na Nipashe, kuhusu utafiti uliofanywa na taasisi hiyo, ili kubaini ukubwa wa tatizo hilo na visababishi vyake.

"Huu ni utafiti mkubwa kuliko yote iliyowahi kufanyika kwenye jamii yetu, ulilenga kupima ukubwa wa tatizo la uzito mkubwa na visababishi vyake. tulipima watu 6691 na tukagundua zaidi ya theluthi mbili yao walikuwa na uzito mkubwa," alisema Dk. Pallangyo.

Alisema utafiti huo ulibaini hayo kwenye utafiti ulifanywa na taasisi hiyo, uliofanyika mwaka huu na kutolewa Septemba 29, mwaka huu.

Alisema sababu za tatizo hilo ni ulaji wa vyakula vya 'fast food', unywaji pombe, kutokuwa na utaratibu kupata kifungua kinywa, unywaji duni wa maji huku kinywaji aina ya soda ukiwa zaidi.

"Kwa ujumla wanawake walikuwa na uzito mkubwa, vitambi, kuliko wanaume. Wenye zaidi ya miaka 40 walionekana kuwa na uzito mkubwa kuliko wenye umri wa chini ya miaka 40," alibainisha Dk. Pedro.

Alisema takwimu duniani zinaonyesha tatizo hilo limeongezeka kwa zaidi ya mara tatu kwa kipindi cha miongo mitatu, na kusababisha kuwa na asilimia 14 ya matatizo ya moyo kushindwa kufanya kazi.




Katibu Tawala wa Wilaya ya Ilala, Chalangwa Selemani (wa pili kushoto), Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam na Zanzibar, Donatus Richard (wa pili kulia) na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingu Pugu Station, Valentine Mhagama (katikati), wakipiga makofi baada ya benki hiyo, kukabidhi meza 35 na viti vyake vyenye thamani ya Sh. milioni 8 kwa ajili ya walimu wa shule hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Meneja wa NMB, Tawi la Ilala, Christine Lifiga na Meneja Mwandamizi Mahusiano ya Serikali, Mkunde Joseph. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kundo: Nichagueni nimalize kero ya umeme, barabara

**Na Happy Severine,** BARIADI

MGOMBEA ubunge Jimbo la Bariadi Andrea Kundo (CCM), amewaomba wananchi wa vijiji vya Itubukilo, Mwanzoya na Halahala Kata ya Itubukilo wampigie kura ili iwe mwisho wa kero ya kutokuwa na umeme pamoja na barabara zisizopitika.

Vijiji hivyo tangu Uhuru vimekosa nishati ya umeme, huku barabara zikishindwa kupitika muda wote hasa kipindi cha masika.

Mgombea huyo alisema endapo atachaguliwa huo ndiyo utakuwa mwisho wa kero hizo.

Kundo alitoa ahadi hizo mbele ya umati wa wananchi wa vijiji hivyo juzi katika mwendelezo wa kampeini zake, ambapo aliwaeleza wananchi hao kama wanataka kutatuliwa kero hizo basi wamchague awe mbunge wao.

Alisema amejionea kero ya barabara inavyowatesa wananchi hao hasa barabara kuu ambayo inaingia na kutoka ndani ya vijiji hivyo, kutoka katika Kata ya Ngulyati, Mwanzoya hadi Kata ya Sakwe.

"Wakati nakuja nimepitia barabara hii, kabla ya kampeni kuanza nilikuja hapa nikaambiwa kero hii, wananchi wengi wanalia na hii barabara, ni kweli hali ni mbaya, hamna barabara, mnateseka sana," alisema.

"Nataka niwaeleze hapa, endapo tarehe Oktoba 28 mtakwenda kufanya kama vile nawaomba, mkinichagua mimi, Diwani wa CCM pamoja na Rais Magufuli, ndiyo utakuwa mwisho wa kero hii," alisema Kundo.

Alisema kazi yake kubwa na ya kwanza kwa wananchi hao endapo atachaguliwa ni kuhakikisha anatengeneza barabara hiyo, ikiwa pamoja na kuleta umeme mara moja ili wananchi hao waweze kujiletea maendeleo.

Akiwa katika Kjiji cha Mwanzoya aliahidi kukamilisha ujenzi wa zahanati ambayo ujenzi wake umeanza kwa nguvu za wananchi, huku katika kijiji cha Itubukilo akiahidi kuongeza watumishi katika zahanati ya kijiji hicho.

## Wakulima korosho sasa watakiwa uhakiki akaunti

**Na Mwandishi wetu,** MASASI

VIONGOZI na wasimamizi wa sekta ya ushirika, wameagizwa kuhakikisha wakulima wa korosho wanahakiki akaunti zao benki katika msimu mpya mwaka 2020/21, ili kuondokana na tatizo la uchelewaji wa malipo ya wakulima.

Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Suleiman Mzee, alitoa agizo hilo alipokuwa akizungumza na Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Charles Malunde, aliyemtembelea ofisini kwake ikiwa ni maandalizi ya msimu huo mpya wa korosho.

Kikao hicho, kililenga kutathmini msimu uliopita ili kuangalia namna bora ya kuondokana na kero zilizojitokeza kwenye Vyama vya Ushirika kwa kufanya maboresho zaidi ya msimu mpya.

Akizungumza kwenye kikao hicho, Mzee alisema uchelewaji wa malipo ya wakulima ni moja ya vikwazo vinavyojitokeza mara kwa mara, hivyo viongozi hao kwa kushirikiana na

benki waratibu zoezi la wakulima kuhakiki taarifa zao.

"Mkulima apate taarifa kwenda kuhakiki taarifa zake za benki ili kama kuna dosari yoyote ipate ufumbuzi mapema kabla ya minada ya mauzo kuanza ili hatimaye apate malipo yake kwa wakati," alisema.

Aidha, Mzee aliwataka viongozi wa ushirika kuendelea kuusimamia na ubora wa korosho zinazokusanywa na wakulima katika vyama vyao.

Aliongeza kuwa ubora huo huanzia hatua za awali kuanzia shambani hadi kufikia ghalani kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa na zinazotolewa na maofisa ugani.

Naye Naibu Mrajis Malunde aliwataka maofisa ushirika, menejimenti na wajumbe wa bodi kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na misingi ya ushirika.

## Asasi yaeleza inavyotoa elimu kwa wapigakura

**Na Gideon Mwakanosya,** NAMTUMBO

ASASI isiyo ya kiserikali ya Mchomoro AIDS Combat Group (MACG) wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma, ambayo imepewa kibali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (MEC) cha kutoa elimu ya mpigakura 2020 mpaka sasa imezifikia kata zaidi ya 10 kati ya kata 21 zilizopo wilayani humo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini Namtumbo, Mkurugenzi Mtendaji wa asasi hiyo, Shazir Malamaye, alisema kuwa mbinu zinazotumika katika kutoa elimu hiyo ni pamoja na kuwa na midahalo mbalimbali iliyokuwa na taarifa yakinifu juu ya elimu ya mpigakura, kusambaza vipeperushi, ngoma za asili pamoja na nyimbo ambazo zina ujumbe wa elimu ya mpigakura.

Malamaye alifafanua zaidi kuwa asasi yake kwa muda wote imekuwa ikihimiza wananchi kushiriki kupigakura Oktoba 28, mwaka huu pamoja na kutangaza kwa kutumia vipaza sauti kijiji hadi kijiji.

Aliishukuru NEC ngazi ya Wilaya ya Namtumbo na taifa, vyombo vya ulinzi na usalama, viongozi wa dini zote na wadau mbalimbali wakiwamo waandishi wa habari.

Alitoa wito kwa wananchi kujitokeza kwa wingi siku ya Oktoba 28 katika vituo walivyojiandikisha ili waweze kupigakura kuwachagua viongozi wanaowataka.

NIPASHE JUMATATU OKTOBA 5, 2020

Nipashe Spotika



WANASOKA 10 WAKUBWA WASIO NA KASI UWANJANI UK. 12&13




# WACHEZAJI WA4 HATIHATI KUPOTEZA NAMBA UNITED

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imekuwa na mwanzo mbaya kwa msimu huu hadi sasa. Mashetani Wekundu hao walilazimika kutegemea mchanganyiko wa bahati na VAR ili kupata ushindi wenye utata wa sekunde ya mwisho kwenye Uwanja wa Amex dhidi ya Brighton Jumamosi iliyopita.

Ishara za mapema za hatari zilionekana katika mchezo wao wa kwanza wa msimu dhidi ya Crystal Palace.

Wakati wa mwanzo mbaya wa United umekuwa kushindwa kwa pamoja kwa timu, utendaji wa wachezaji wengine umeibua maswali mengi juu ya uwepo wao kwenye timu. Ingawa kikosi cha United sio kikubwa zaidi, Kocha Ole Gunnar Solskjaer anaweza kupoteza uvumilivu wake kwa wachache ambao wanaishusha timu yake. Leo, tunaangalia wachezaji wanne wa Manchester United ambao wanahitaji kuongeza bidii uwanjani ikiwa wanataka kuimarisha nafasi yao katika timu hiyo.

**4: ANTHONY MARTIAL**

Mfaransa huyo bila shaka alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi wa Manchester United msimu uliopita. Martial aliwapambania Mashetani Wekundu hao hadi kumaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu England msimu uliopita, akifunga mabao muhimu.

Alithibitisha imani yake kwa Solskjaer, akifanikiwa kama mshambuliaji, na kufikia hesabu ya juu zaidi ya kazi yake. Hiyo ilisababisha kurudi katika kikosi cha Timu ya Taifa ya Ufaransa, ambacho alikuwa nje kwa muda mrefu. Kwa bahati mbaya, Mfaransa huyo ameshindwa kutunza kiwango chake cha msimu uliopita hadi sasa.

**3: AARON WAN-BISSAKA**

Kila mtu alikuwa akifurahi kuhusu Aaron Wan-Bissaka msimu uliopita. Hakuwa Trent Alexander-Arnold, kwani alikuwa mmoja wa wachezaji bora kwenye ligi. Alikuwa na kasi, haraka na mwenye nguvu. Mwingereza huyo. Alikuwa mmoja ya sababu kwa nini United ilisimamia rekodi nzuri ya kujihami msimu uliopita.

Hatua kutoka Crystal Palace kwenda Manchester United inaweza kuwa kubwa kwa wachezaji wengi wachanga na ilidhaniwa kwamba Mwingereza huyo ataboresha uchezaji wake msimu huu. Lakini kiwango chake katika michezo miwili ya kwanza kimeibua wasiwasi kidogo kwa United.

**2: PAUL POGBA**

Paul Pogba amekuwa Manchester United kwa misimu mitano sasa na bado hatujamwona akitawala kweli dimba mara kwa mara. Kitaalamu, Mfaransa huyo ana talanta ya kuwa mchezaji bora kwenye Ligi Kuu England na uwepo wake tu unapaswa kutimiza mahitaji ya ubunifu wa timu yake. Lakini Pogba aliyekiwasha sana kule Turin akiwa na Juventus si huyu wa pale Old Trafford.

Mfaransa huyo alikuwa na nusu ya kwanza ngumu ya msimu wa 2019/20, lakini alionekana kufufuka tangu kuwasili kwa Bruno Fernandes. Alionekana kuishi kwa nguvu na akili ya Mreno huyo na safu ya kiungo ya United ilionekana kuwa imara zaidi.

Lakini baada ya michezo miwili ya kwanza ya msimu mpya, Pogba anaendelea kuzuiliwa na shida zile zile ambazo zimemrudisha Old Trafford. Anakosa ushupavu kidogo.

**1: VICTOR LINDELOF**

Siku za Lindelof pale Manchester United zinaweza kuhesabiwa.

Raia huyo wa Sweden ambaye alijiunga na timu hiyo majira ya joto mwaka 2017 chini ya Jose Mourinho, ameshindwa kutekeleza matarajio.

Inaonekana ni suala la muda tu kabla ya Lindelof kurudishwa kwenye benchi. Lakini mambo yanaweza kuwa mabaya kwa Msweden huyo kwani kurudi kwa Tuanzebe karibu kutoka kwa jeraha kunaweza kumweka chini ya huzuni zaidi. Na ndio sababu Lindelof lazima atoe jasho kwenye mafunzo na kurudisha kiwango chake bora.

## ISIKUPITE

NAHODHA na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Mbwana Samatta, amefunga mabao mawili katika mechi yake ya kwanza akiwa na Fenerbahçe katika mechi ya Ligi Kuu Uturuki dhidi ya Fatih Karagumruk. Fenerbahce ilishinda mabao 2-1.



Extra Time

# WANASOKA 10 WAKUBWA WASIO NA KASI UWANJANI

**LONDON, Uingereza**

SOKA la kisasa limeona mkazo zaidi ukiwekwa kwa wachezaji wenye kasi. Kwa ujumla, wachezaji kama hao wanapendeza zaidi kuwatazama, na nyota kama Adama Traore wa Wolverhampton Wanderers akiingia akilini; anachanganya kwa kasi ya ajabu na uwezo wa kupiga chenga.

Wasimamizi siku hizi wanapendelea wachezaji kama hao. Uwezo wa kukimbia au kupiga chenga kupitia mpinzani unafurahisha; pia ni uthibitisho wa asili wa ubora, na mawinga kama Eden Hazard na Raheem Sterling wakithibitisha hivyo.

Lakini, kuna wachezaji fulani wenye uwezo wa kucheza kwa kiwango cha juu licha ya kuwa hawana kasi kama hiyo. Wanategemea zaidi ustadi wao wa kiufundi na kulinganisha akili ili kufidia ukosefu huu wa kasi, na kuamuru kucheza kutoka kwa nafasi za kina na kuchukua kwa usahihi.

Makala hii inawachambua wachezaji 10 wakubwa ambao hawana kasi

**10: GRANIT XHAKA - ARSENAL**

Granit Xhaka kwa mara nyingine tena amekuwa mchezaji muhimu katika klabu ya Arsenal chini ya usimamizi wa Mikel Arteta.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uswisi alijiunga na Arsenal akitokea Borussia Monchengladbach mwaka 2016, kwa euro milioni 45, na katika miaka iliyofuata alifurahi sana akiwa Emirates. Xhaka amekuwa mmoja wa viungo bora wa Arsenal, lakini hajafurahia uhusiano mchanganyiko na mashabiki.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 amepata mkataba mpya wa maisha chini ya Arteta, na ushawishi wake umeonekana uwanjani. Mpitaji mzuri na pia mpokeaji mzuri wa Xhaka anaonekana kuwa na jukumu muhimu msimu huu pia.

**9: JOAO MOUTINHO - WOLVES**

Mmoja wa viungo wa chini sana, Joao Moutinho amekuwa kimya kimya na kuwa mmoja wa wachezaji bora wa Wolverhampton Wanderers tangu ajiunge na klabu hiyo.

Baada ya kuigharimu Wolves euro milioni sita kutoka AS Monaco mwaka, 2018, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 amekuwa akiwakilisha vyema safu ya kiungo. Akifanya kama mshauri kwa kiungo mwenzake wa Ureno, Ruben Neves, Moutinho na amekuwa muhimu kwa jinsi kikosi cha Nuno Espirito Santo kinavyofanya kazi.

Wakati klabu imekuwa ikifanya kazi wakati huu wa uhamisho, hawajaimarisha nafasi za kiungo, na inaonekana kuna uwezekano kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno atakuwa mchezaji muhimu licha ya umri wake.

**8: OLIVIER GIROUD - CHELSEA**

Olivier Giroud anaweza kuwa sio mchezaji aliye na kipaji zaidi uwanjani, lakini kuna sababu anakaa nambari tisa inayopendelea ya Ufaransa mbele ya Anthony Martial.

Kijana huyo wa miaka 34 ni mwendeshaji asiyejitolea, akipendelea kuchukua watetezi ili kuruhusu wachezaji wenzake wenye talanta na wa haraka kupata nafasi na kufunga mabao. Giroud ana rekodi nzuri ya kufunga mabao yake mwenyewe; akifunga kwa kiwango sawa kwa Arsenal na sasa kwa Chelsea.

Kuwasili kwa Timo Werner na kuibuka kwa Tammy Abraham kunaweza kupunguza dakika zake, lakini bado ni chaguo bora kutoka benchi. Inter Milan walikuwa na nia ya kumsajili msimu huu, huo ni moja ya ushahidi wa ubora wake.

**7: HARRY MAGUIRE - MANCHESTER UNITED**

Harry Maguire mara nyingi amekuwa akikosolewa bila haki wakati wake akicheza pale Manchester United, lakini ukweli unabaki nyongeza yake imefanya safu ya nyuma kuwa imara zaidi.

Maguire alijiunga na Manchester United kutoka Leicester City mnamo 2019 kwa euro milioni 87, na kumfanya kuwa mlinzi ghali zaidi wa wakati wote. Na amekuwa nahodha wao kuanzia Januari hii baada ya kuondoka kwa Ashley Young kwenda Inter Milan.

Ingawa kumekuwa na makosa, mchezaji huyo wa kimataifa wa Uingereza ameonekana mzuri kwa msimu mwingine, na uwezo wake wa kucheza mpira ni muhimu kwa kocha Ole Gunnar Solskjaer.

**6: JORGINHO - CHELSEA**

Kwa msimu mwingine wa joto, ilionekana kama wakati wa Jorginho huko Chelsea ulikuwa umefikia mwisho.

Kuibuka kwa kijana Billy Gilmour kulimfanya Jorginho kuwa mchezaji wa benchi, na kulikuwa na uvumi kwamba atauzwa. Lakini anaendelea kuwa sehemu ya kikosi cha Frank Lampard, na mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia anaonekana uwezekano wa kuondoka klabuni hapo haupo, huku Ross Barkley akiwa tayari ameondoka.

Alijiunga na Chelsea mnamo 2018 kwa euro milioni 57, nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 ni mmoja wa wachezaji wazoefu zaidi wa kikosi cha vijana cha Chelsea, na Lampard anatumaini kuwa atawasaidia.

**5: BUSQUETS ZA SERGIO - BARCELONA**

Kwa muda mrefu anayetajwa kama mchezaji aliyepungukiwa zaidi katika mpira wa miguu ulimwenguni, Sergio Busquets ni wazi sio mchezaji aliyewahi kuwa.

Mmoja wa viungo bora wa ulinzi aliyecheza mchezo huo, mchezaji huyo wa Hispania sasa anaonekana kama dhima badala ya mali. Lakini Busquets, ambaye ametumia muda wake wote kucheza huko Barcelona, anaonekana kuwa na nia ya kudhibitisha kwamba sivyo ilivyo.

Katika umri wake wa miaka 32 amependwa na wachezaji kama Johan Cruyff na Vicente del Bosque kwa mtindo wake wa uchezaji, na huenda akamaliza kipindi chake cha uchezaji akiwa Barcelona, ambapo amecheza karibu mechi 600 kwenye mashindano yote tangu aanze kucheza 2008.

**4: MICHEZO HUMMELS - BORUSSIA DORTMUND**

Mmoja wa walinzi bora duniani, Mats Hummels anaendelea kuchukua jukumu muhimu kwa Borussia Dortmund.

Hummels alijiunga tena na Borussia Dortmund kutoka Bayern Munich kwa euro milioni 30.5 mnamo mwaka 2019, baada ya kucheza zaidi ya mechi 300 kwenye mashindano yote wakati wa kipindi chake cha kwanza kwenye klabu hiyo. Nyota huyo wa miaka 31 amepewa dhamana ya kuongoza mabeki wachanga kama Manuel Akanji na Dan-Axel Zagadou, wakati akicheza dakika za maana.

**3: LUKA MODRIC - REAL MADRID**

Mmoja wa viungo bora wa kizazi hiki, Luka Modric aliimarisha urithi wake kwa kushinda Ballon d'Or mnamo mwaka 2018.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia, aliyejiunga na Real Madrid mwaka 2012 akitokea Tottenham Hotspur kwa euro milioni 35, anasifika kwa ubunifu wake, kufaulu na uwezo wa kiufundi. Ushirikiano wa kati wa Modric na Toni Kroos uliunda msingi wa Madrid waliposhinda mataji matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu mfululizo.

Sasa akiwa na umri wa miaka 35, Modric ameonyesha dalili za kupungua. Licha ya hayo, alicheza mechi 40 kwenye mashindano yote kwa Los Blancos msimu uliopita, waliposhinda taji la ligi.

**2: THOMAS MULLER - BAYERN MUNICH**


Thomas Muller anaweza kuwa hafurahishi machoni, lakini ufanisi wake na maonyesho thabiti yanaweza kulinganishwa na wachache tu.

Ana uwezo wa kucheza katika nafasi tofauti za ushambuliaji, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani amesifiwa sana kwa akili yake ya mechi, mwamko wa nafasi na uwezo wa harakati za nje ya mpira.

1: TONI KROOS - REAL MADRID

Toni Kroos ni mmoja wa viungo bora kwenye mpira wa miguu hivi sasa.

Kroos alijiunga na Real Madrid kutoka Bayern Munich mwaka 2014 kwa euro milioni 25, na ameendelea kucheza karibu mechi 300 katika mashindano yote ya Los Blancos hao.



Jorginho




Harry-Maguire

## Nukuu

"Nafikiri alikuwa vizuri. Nafikiri aliokoa hatari nyingi na kucheza vizuri sana. Alionyesha kuwa ana uwezo mkubwa na kiukweli atakuwa msaada mkubwa kwa timu yetu. Nimefurahishwa na kiwango chake na alionekana kama vile ameshacheza hapa kwa muda mrefu." **Kocha wa Chelsea, Frank Lampard akizungumzia kiwango cha golikipa, Eduardo Mendy.**



"Baada ya mambo mengi, ningependa kumaliza kila kitu hapa. Tunatakiwa kuungana ili kuhakikisha timu inakuwa na mafanikio kwa msimu huu. Kwa sasa mimi akili yangu ni kutaka Barcelona iwe na mafanikio makubwa msimu huu," **Lionel Messi, mshindi mara sita wa Ballon d'Or alisema.**



"Kwa hakika nina furaha na kiwango cha wachezaji wangu, na hilo linafanya benchi la ufundi kuwa kwenye wakati mgumu kuchagua kikosi. Unaweza kuona wachezaji wanabadilika kila wiki, ni vigumu kwa kila wiki mchezaji kupata nafasi na sio kwa Mesut (Ozil) tu bali na kwa wachezaji wengine." **Mikel Arteta, Kocha wa Arsenal alibainisha.**



# OGOPA YANGA KIPINDI CHA PILI

**Na Adam Fungamwango**

MAKOCHA wa timu za Ligi Kuu Tanzania Bara sasa wana kibarua cha kutengeneza mfumo, au mkakati kwa klabu wanazozifundisha wa kuizuia Yanga isipate goli kipindi cha pili.

Imeonekana kuwa timu hiyo ni hatari zaidi ikiingia kipindi cha pili, kuliko cha kwanza kwa mujibu wa takwimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu tulizonazo.

Ushindi wa mabao 3-0 ilioupata juzi Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Coastal Union umewafanya mabingwa hao wa zamani kuendeleza rekodi yao ya kuwa wakali zaidi kipindi cha pili.

Katika mechi zao za Ligi Kuu Tanzania Bara ilizocheza, Yanga imeshinda mechi nne na kutoka sare moja na mechi zote ilizoibuka na ushindi mabao yake yamefungwa kipindi cha pili.

Ni mechi moja tu ambayo Yanga imefunga bao kipindi cha kwanza kwenye Ligi Kuu. Na hata hivyo haikuibuka na ushindi katika mchezo huo.

Ilikuwa mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Septemba 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ilipocheza dhidi ya 'Maafande' wa Prisons.

Kwenye mechi hiyo, Yanga ilifunga bao kipindi cha kwanza, dakika ya 18 likiwekwa wavuni na Michael Sarpong.

Lilikuwa ni bao la kusawazisha dhidi ya lile la Prisons lililofungwa dakika ya saba tu na Lambart Subianka na mechi iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1.

Baada ya hapo Yanga imeshinda mechi nne mfululizo, huku mabao yao yote yakiwekwa nyavuni kipindi cha pili.

**1. Yanga 1-0 Mbeya City (dk 85)**

Mechi ya kwanza ya Yanga kushinda msimu huu ilichezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Septemba 13, mwaka huu na ilicheza dhidi ya Mbeya City.

Katika mechi hiyo, Yanga iliibuka na ushindi wa bao 1-0. Ni bao lililofungwa kipindi cha pili.

Ilibaki dakika tano tu mechi hiyo kumalizika, huku baadhi ya mashabiki wenye roho ndogo wakiwa wameshaanza kutoka.

Kona iliyochongwa na Carlos Carlinhos ilitua kichwani mwa Lamine Moro akaiweka wavuni na kuifanya timu hiyo kuibuka na ushindi huo.




Lamine

**JE, WAJUA?**



KOCHA wa Crystal Palace, Roy Hodgson amepoteza mechi sita mfululizo za Ligi Kuu England zilizochezwa kwenye Uwanja wa Stamford Bridge tangu aliposhinda kwa mara ya kwanza akiwa na Blackburn Aprili mwaka 1998. Hodson juzi alikula kichapo cha mabao 4-0 kwenye uwanja huo.

**2. Yanga 1-0 Kagera Sugar (dk 72)**

Hii ilikuwa kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba mkoani Kagera. Yanga ikicheza mechi ya kwanza ugenini ilikutana na mechi ngumu Septemba 19, mwaka huu, lakini mwisho wa siku ikaibuka na ushindi wa bao 1-0 na kuipa pointi tatu muhimu kwenye mechi ya raundi ya tatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Bao pekee kwenye mechi hiyo nalo lilifungwa kipindi cha pili.

Dakika 18 kabla ya pambano kumalizika, kiungo aliyesajiliwa na klabu hiyo akitokea AS Vita, Mukoko Tonombe aliifungia timu yake bao pekee, baada ya kupokea mpira wa krosi kutoka kwa mchezaji mwenzake kutoka timu hiyo ya zamani, Tuisila Kisinda na kuujaza wavuni, Yanga ikashinda mechi ya pili mfululizo.

**3. Yanga 1-0 Mtibwa Sugar (dk 61)**

Septemba 27, mwaka huu, Yanga ilikwenda kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro kucheza dhidi ya Mtibwa Sugar.

Ilikuwa ni mechi ya raundi ya nne ya Ligi Kuu Tanzania Bara. Ilifanikiwa kupata ushindi wa tatu mfululizo, lakini ukiwa ni wa pili kwenye uwanja wa ugenini.

Iliichapa Mtibwa Sugar bao 1-0, ambalo nalo vile vile lilifungwa kipindi cha pili. Ilikuwa ni dakika ya 61, Lamine alipofunga bao hilo. Kama kawaida aliunganisha kwa mguu mpira wa kona uliopigwa na Carlinhos na kuendeleza rekodi yao ya kufunga mabao kipindi cha pili.

**4. Yanga 3-0 Coastal (dk 47, 52, 63)**

Jumamosi iliyopita Yanga ilirejea nyumbani baada ya mechi mbili mfululizo wa ugenini ambazo zote ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar na Mtibwa Sugar.

Kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ilikuwa mwenyeji wa Coatal Union kutoka Tanga, Yanga ikishinda mabao 3-0.

Mabao yote matatu yalifungwa kipindi cha pili. Dakika mbili tu baada ya mapumziko kiungo Muangola, Carlinhos alifunga bao kwa kichwa liloonekana kuwachanganya wachezaji wa Coastal Union.

Haruna Niyonzima aliongeza bao la pili dakika ya 52, kabla ya Yacouba Songne kutupia bao la tatu kwenye dakika ya 63, ushindi ulioiongezea Yanga pointi na kufikisha jumla ya 13, ikishinda mechi nne na sare moja, lakini takwimu zikisomeka kuwa magoli sita kati ya saba iliyokuwa nayo, iliyofunga kwenye mechi zote nne ilizoshinda Yanga, yamefungwa kipindi cha pili.



# Azaki kuwekewa mazingira wezeshi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MSAJILI wa mashirika yasiyo ya kiserikali nchini, Vickness Mayao, amesema serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi na kushirikiana na asasi za kiraia (Azaki) endapo zitafuata misingi iliyokusudiwa.

Mayao alibainisha hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizindua ofisi ndogo ya Foundationa for Civil Society na kituo cha azaki zilizopo katika eneo la Area 'C' jijini Dodoma.

Alizitaka asasi hizo kufanya kazi kwa kufuata misingi inayoziongoza bila kukiuka misingi yake ikiwamo kufanya kazi kwa ushirikiano katika kuhudumia wananchi ili wapate maendeleo.

Alisema kuwa serikali inatambua mchango mkubwa unaofanywa na asasi hizo na kuahidi kuwa serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa mashirika hayo kufanya kazi zao na kuwa kiunganishi kati ya maendeleo na wananchi.

"Serikali imeweka mazingira mazuri na wezeshi kwa mashirika na asasi za kiraia kufanya kazi na tumeweka miongozo itakayowezesha asasi na mashirika hayo kufanya kazi zao," Mayoa.

Aidha, alisema kuwa ofisi na kituo cha azaki zitasaidia upatikanaji wa taarifa na maarifa muhimu kuhusu asasi hizo kwa wananchi na serikali kwa wakati.

"Mashirika haya yamekuwa na mchango mkubwa katika kuleta maendeleo kwa wananchi na kusaidia kuondokana na umaskini, hivyo serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi na kushirikiana nao," alisema Mayoa.

Kwa upande wake, Rais wa asasi za kiraia nchini, Dk. Stigmata Tenga, alisema tangu kuanza kufanya kazi kwa azaki miaka 18 iliyopita nchini, wametoa ruzuku kwa mashirika 6,000 na kuziwezesha asasi 10,000 katika kutekeleza majukumu yao nchini.

Tenga aliongeza kuwa kufunguliwa kwa ofisi hiyo kutawezesha kwa kila mtu atakayepata nafasi ya kutembelea kituo hicho atakutana na wadau wengine wa maendeleo na kupata taarifa, kujifunza na kukuza ushirikiano ndani ya sekta ya azaki.




Ofisa Mradi wa Elimu Jumuishi kutoka kitengo cha Kanisa la Free Pentecostal of Tanzania (FPCT), jijini Dodoma, Jane Mgidange, akitoa elimu ya kampeni ya ushawishi na utetezi kwa ajili ya watoto wenye ulemavu kwa wananchi wa Wilaya ya Bahi juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wasafirishaji watalii wahimizwa uadilifu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki, amewataka wanaotoa huduma ya kusafirisha watalii nchini kuwa waaminifu na kuboresha huduma zao ili kuwavutia watalii.

Dk. Nzuki aliyasema hayo mwishoni mwa wili alipokutana na ujumbe kutoka Taasisi ya Sekta Binafsi nchini (TPSF) walipomtembelea ofisini kwake.

Alisema licha ya serikali kuboresha vyuo vya kufundisha watoa huduma za utalii nchini bado kuna kundi la watoa huduma za usafiri kwa watalii walisahaulika, hivyo wanahitaji elimu ya kuwapokea wageni wanapofika na kutembelea vivutio.

Katibu huyo alisema kwa sasa watoa huduma hizo hawana vifaa vinavyoonyesha kilomita anazotembea wakati wa kutoa huduma za usafiri ili kuondoa utata wa bei za usafiri. "Mnatakiwa kuwa na uwazi kwa kuweka bei za kila kilomita moja anayotembea ili mtumiaji akipokelewa na kusafiri hadi eneo analokwenda ajue bei halisi," alisema.

Aidha, alisema serikali inaendelea na mpango wa kuboresha mitaala ya kufundishia kwa wanafunzi wa masomo ya utalii, ili kuweka usawa katika kuwapima wanafunzi hao.

"Tuna kazi ya kuhuisha mitaala yetu ya kufundishia wanafunzi wa vyuo vya utalii ili mwisho watakuwa na eneo maalumu la kuwapima uwezo wao baada ya kuhitimu," alisema.

Kwa upande wake mwakilishi wa Mkurugenzi wa Sekta Binafsi, Richard Komba, alisema katika kutimiza azma ya kuboresha biashara nchini, TPSF kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wanatekeleza mkakati wa taifa wa kuendeleza ujuzi kupitia mradi wa kukuza stadi za kazi na ujuzi.

Komba alisema katika mradi huu TPSF wamepewa jukumu la kuanzisha mabaraza ya ujuzi ya kisekta ambapo sekta sita zimepewa kipaumbele ambazo ni kilimo, utalii, TEHAMA, ujenzi, uchukuzi na nishati.

"Lengo la kuundwa kwa mabaraza ya ujuzi ya kisekta ni kuwaleta pamoja wadau wote kutoka sekta binafsi na sekta ya umma ili kujadiliana namna bora ya kuboresha nguvu kazi nchini," alisema.

Alibainisha kuwa kwa miaka mingi waajiri nchini wamekuwa wakipata tatizo kubwa la kupata rasilimali watu yenye ujuzi inayohitajika katika kutekeleza majukumu yao na hivyo kusababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa biashara.

Alisema kutokana na waajiri kukosa vijana wenye sifa hulazimika kutafuta wataalamu wenye ujuzi stahiki kutoka nje ya nchi au kutumia fedha nyingi katika kugharamia mafunzo kwa watumishi katika sehemu za kazi.

# Wazazi watakiwa kufichua watoto wenye ulemavu

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

WAKAZI wa Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, wametakiwa kuwafichua watoto wenye ulemavu, ili wapatiwe misaada ya kielimu na huduma za afya.

Ofisa Mradi wa Elimu Jumuishi kutoka Kitengo cha Kanisa la Free Pentecostal of Tanzania (FPCT) Jiji la Dodoma na Wilaya ya Bahi, Jane Mgidange, alitoa wito huo juzi alipokuwa akizungumza na wakazi hao kwenye kampeni ya ushawishi na utetezi kwa ajili ya elimu jumuishi juu ya haki za mtoto.

Alisema kuwaficha majumbani watoto hao ni kuwafanyia ukatili mkubwa kwa kuwanyima haki zao za kimsingi na kuwaongezea ugumu wa maisha.

Alieleza kuwa kama wangewaibua na kupatiwa misaada mbalimbali ingepunguza makali katika maisha yao.

"Naomba niwaambie ukweli wazazi na walezi wangu nyinyi pamoja na wananchi wa hapa Bahi msiwe waoga wala hofu ya kuwafichua watoto wenye ulemavu, mkifanya hivyo mtakuwa mkiwazuia hata na vipawa walivyokuwanavyo," alisema.

Aliongeza: "Mifano tunayo leo hii ndani ya serikali tuna watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali na wana nafasi kubwa hivyo ninawaomba waibueni ili wapate misaada."

Ofisa huyo aliwaasa kuondokana na dhana potofu iliyojengeka kwa jamii kufikiri kuwa watoto wenye ulemavu ni laana au mkosi.

"Hii siyo kweli bali ni sababu mbalimbali zinazotokana na sababu mbalimbali kama vile lishe duni, ulevi, afya na hata na kunyimwa elimu," alisema.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mradi wa ulemavu kutoka FPCT, Makao Makuu Dar es salaam, Lucas Mhenga, alisema kuwa jukumu la mradi huo ni kuhakikisha kuwa watoto wenye ulemavu wanapata stahiki zao ikiwamo elimu, matibabu, chakula, mavazi na kutengenezewa miundombinu rafiki.

Naye, Ofisa Tarafa ya Bahi, Maiko Nkunya, alisema serikali itahakikisha inatoa ushirikiano wa kutosha kwa kanisa hilo ili watoto wenye ulemavu wapate haki zao za msingi.





## Makundi maalum yaahidiwa mikopo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imeahidi kuendelea kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa makundi ya wanawake, vijana na walemavu ili waweze kujiajiri na kuongeza kipato kupitia shughuli wanazozifanya.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Ofisa Maendeleo wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Vincent Msola, wakati akizungumza na Nipashe juu ya namna wanavyoendelea kutoa mikopo kwa makundi hayo, ili waweze kujikwamua na umaskini na kuweza kuendesha maisha yao.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau imejitahidi kutoa mafunzo ya namna ya kuzalisha na kuandaa bidhaa pamoja na kuwaunganisha kwenye vikundi ili kukidhi vigezo vya kupata mikopo kutoka halmashauri.

Alitaja moja ya wadau kutoka Halmashauri ya Jiji ambo wamehamasisha makundi ya vijana na wanawake kupata mikopo ni Shirika la Elimisha ambalo linajihusisha na masuala ya kutoa elimu ya upangaji bajeti kuanzia ngazi ya familia.

"Serikali inatambua umuhimu wa hatua ya shirika hilo la Elimisha kuja na mkakati wa kutoa elimu na mafunzo ambayo yatachangia wasichana hao kujiajiri na kuendesha shughuli ya uzalishaji pamoja ili kuondokana na umaskini na hii imesaidia vijana, wanawake na watu wenye ulemavu sasa kujiunga kwenye vikundi," alisema Msola.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Ilemi, Mwanaisha Rashid, alisema kama serikali ya mtaa watahakikisha wanashirikiana na Shirika hilo la Elimisha katika kuwatambua wasichana katika mtaa wao ambao wanauhitaji wa kupewa mafunzo ya kuweza kujiongezea kipato.

Alisema kuna tatizo kwa baadhi ya wasichana kukata tamaa kutokana na kutokuwa na maarifa ya kujiongezea kipato na kuwa uamuzi wa shirika hilo kutoa elimu ya kuwawezesha wasichana kujikwamua katika maisha umekuja kwa wakati mwafaka.

Mkurugenzi wa Shirika la Elimisha, Festo Sikagonamo, alisema malengo ya shirika ni kuhakikisha linatoa elimu ya kuwajengea uwezo wa kijipatia kipato wasichana ambao baadhi yao wapo majumbani na hawana cha kufanya.

Alisema lengo la msingi kutoa mafunzo hayo ni kuwawezesha wasichana hao kuwa na maisha bora yanayochangiwa na ushiriki wa wasichana katika kuongeza kipato, uwezo binafsi wa wasichana hao kujiendesha na kuwa na uchumi endelevu pamoja na kuwa na mchango mkubwa katika elimu na maendeleo ya watoto.

Alisema kuwa shirika limejipanga kushirikiana na viongozi wa serikali kuhakikisha wasichana waliopo katika ngazi za mitaa wanaufaika na elimu ya kujiongezea shughuli za kiuchumi.

# Ujangili wa tembo wapungua Kusini

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

VITENDO vya ujangili katika hifadhi za Taifa za Ruaha, Kitulo na Katavi katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini vimepungua kwa kiasi kikubwa.

Imeelezwa kuwa hakuna mizoga ya tembo iliyokutwa ndani ya hifadhi hizo kwa miaka miwili mfululizo vinavyotokana na viashiria vya ujangili.

Kamishna wa uhifadhi Kanda ya kusini, Pius Mzimbe, aliyasema hayo juzi wakati wa mahojiano wa waandishi wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET) chini ya Ufadhili wa Shirika la Marekani la (USAID), ambao walitembelea maeneo mbalimbali ya vijiji na uhifadhi kwa lengo la kuangalia namna wananchi wanaozunguka Hifadhi ya Ruaha wanashikiri katika kudhibiti vitendo vya ujangili na manufaa wanayoyapata juu ya ujirani mwema kati yao na hifadhi.

Alisema hivi sana katika hifadhi hizo kuna askari wa kutosha na vifaa vya kisasa kwa ajili ya kukabiliana na ujangili na kwamba licha ya kuwapo mitandao iliyokuwa inajihusisha na ujangili, lakini TANAPA wamejitahidi kudhibiti kwa kufanya misako na kufanikiwa kuwakamata majangili na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Aliongeza kuwa serikali imejitahidi kuweka nguvu kubwa katika kukabiliana na vitendo vya ujangili katika hifadhi na hali ya ujangili imepungua na wanyama kama tembo, nyati na twiga wanazidi kuzaliana kwa kasi kutokana na kuishi kwa amani ndani ya hifadhi.

Aidha, alisema kumekuwa na udhibiti mkubwa wa ujangili unaotokana na uvunaji wa zao la chikanda katika hifadhi ya taifa ya kitulo kwa sababu ya zao hilo miaka ya nyuma kuwa na soko kubwa katika maeneo mbalimbali ya nchi na nchi jirani za kusini mwa Tanzania. Alisema zamani kulikuwa na mtandao wa majangili wa zao la chikanda uliokuwa unajumuisha wafanyabiashara waliokuwa wanasafirisha zao hilo katika maeneo tofauti ya nchi na nchi jirani za kusini mwa Tanzania, lakini sasa hali ni salama kutokana na askari kufanya doria muda wote ndani ya hifadhi na ushirikiano mzuri na wananchi wanaoishi karibu na hifadhi hizo. "Kulikuwa na ujangili wa kutisha wa uvunaji wa zao la chikanda katika Hifadhi ya Kitulo miaka ya nyuma, kutokana na madai ya zao hilo kupendwa sana ndani na nje ya nchi, lakini kwa sasa imebaki hisitoria kutokana na majangili wa zao hilo kutokomezwa kabisa," alisema Dk. Timbuka.

Alisema mbali na uwapo wa askari waliopewa mafunzo ya kutosha na vifaa vya kisasa vya kukabiliana na ujangili, kumekuwa na ushirikiano mzuri na wananchi wanaoishi karibu na hifadhi katika mapambano ya kutokomeza majangili.

Aliongeza kuwa ujangili wa wanyama kama tembo umebaki historia katika hifadhi za taifa za Ruaha na Katavi katika ukanda wa kusini kwa kuwa kuna doria na msako wa njia mbalimbali ukiwapo wa kutumia ndege na askari wanaotumia magari.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, alisema wamejitahidi kushirikiana na TANAPA kudhibiti vitendo vya ujangili na mapigano kati ya wahifadhi na wananchi kwa kutoa elimu juu ya utunzaji wa hifadhi na kutoingia katika hifadhi kulisha mifugo kama vile ng'ombe na mbuzi pamoja na kutovua samaki.

Aliwakumbusha wananchi kuendelea kutoa taarifa wanyama wanapovamia maeneo yao na kuharibu mazao na kujeruhi watu.



Ofisa wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) katika Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, Silas Meshilieki (kushoto), akitoa mafunzo ya ufugaji wa nyuki wa kisasa kwa vikundi vitano, yaliyowezeshwa na kampuni ya uchimbaji madini ya Shanta Gold Mine (New Luika), wilayani humo, mwishoni mwa wiki, kwa lengo la kuongeza maarifa yatayowasaidia kuzalisha kwa tija ili kunufaika na ufugaji huo. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mbarali yajenga shule 6 za sekondari

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

SERIKALI kwa kushirikiana na wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, imefanikiwa kujenga shule sita za sekondari, lengo ni kutoa fursa kwa wanafunzi wanaofaulu mitihani ya darasa la saba, kupata nafasi ya kuendelea na sekondari.

Aidha, shule hizo zimejengwa ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa lililojitokeza baada ya idadi kubwa ya wanafunzi kutakiwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya hiyo, Ruben Mfune, alipozungumza na Nipashe, ambapo alibainisha kuwa wananchi wengi wamekuwa na mwamko mkubwa wa kuunga mkono juhudi za serikali za kuhakikisha wanafunzi wanasoma kwenye mazingira mazuri.

Mfune alisema shule zilizojengwa kwa nguvu ya serikali na wananchi ni Muwale yenye madarasa matano, Kapunga yenye madarasa matatu, Itamboleo yenye madarasa vitatu, Ihanga yenye madarasa matano na Nyamakuyu yenye madarasa vitano.

Alisema ujenzi wa shule hizo ni mwendelezo wa ujenzi wa shule za sekondari na vyumba vya madarasa kwa shule zilizopo na kuwa kwa mwaka 2019, serikali kwa kushirikiana na wananchi walijenga shule mbili ambazo Ipwani ambayo ilikuwa na madarasa vitatu na kuwa kwa mwaka huu wameongeza ujenzi wa madarasa mawili. Shule nyingine iliyojengwa mwaka jana Mwakaganga iliyokuwa na vyumba vitano na kuwa kwa mwaka huu wameongeza vyumba vingine vitano na kuwa mpango uliopo kwa mwaka ujao ni kujenga shule zingine tatu za sekondari.

Alisema jitihada za ujenzi huo unatokana na mwamko wa wananchi kutambua mchango wa serikali katika kutoa elimu bure kwa wanafunzi kuanzia shule za awali mpaka shule za sekondari nchini kote.

Alisema mafanikio ya ujenzi wa shule hizo unatokana na michango ya hiari ya wananchi katika kuharakisha sekta ya elimu wilayani humo pamoja na mipango thabiti ya wilaya katika kuondokana na changamoto ya wanafunzi wanaokosa elimu kwa sababu ambao zipo ndani ya uwezo wa wilaya.

Pia wilaya hiyo tulifanikiwa kuendesha harambee ya wadau mbalimbali wa elimu kuchangia ujenzi wa shule hizo mpya sita za sekondari na ujenzi wa vyumba vingine 36, ambavyo vilikuwa vinahitajika kwa ajili ya wanafunzi waliokosa nafasi baada ya kuchaguliwa ambapo kiasi cha Sh. milioni 151 na vifaa vilipatikana.

Aliwaomba wananchi kuendelea kujitolea kwa ajili ya shughuli za ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa kuamini kuwa inawezekana tatizo la vyumba vya madarasa na madawati linaweza kuwa historia kwa sababu wilaya hiyo inajitosheleza katika masuala ya kiuchumi kutokana na kilimo cha zao la mpunga.



# ZEC kusimamia uchaguzi kwa amani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), imesema itaendelea kushirikiana na wadau wa uchaguzi, ili kuhakikisha Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 27 kwa kura ya mapema na Oktoba 28, unafanyika kwa salama na amani.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mkuu mstaafu Hamid Mahmoud Hamid, alisema hayo wakati akizungumza na viongozi wa dini kisiwani Pemba.

Alisema, tangu kuanza kwa matayarisho ya hatua mbalimbali za uchaguzi, ZEC imekuwa karibu na wadau wake kwa kufanya mikutano mbalimbali ili amani na utulivu iendelee kudumu kabla na baada ya uchaguzi.

Aliwataka viongozi wa dini waendelee kuhamasisha kampeni na hatua nyingine za uchaguzi kwa utulivu na amani ili nchi iendelee kuwa visiwa vya amani.

Alisema, katika kuzingatia nafasi ya viongozi hao katika jamii iliyowazunguka, Tume imeona kuwa wao ni wadau muhimu wa uchaguzi na inatambua umuhimu wao kwa vile wanaongoza kundi kubwa katika jamii.

Jaji Mahamoud, aliwaomba viongozi hao kuendelea kuhubiri amani kwa wananchi wote, kabla na baada ya uchaguzi pia kuendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa jamii ili iweze kushiriki kikamilifu katika masuala ya uchaguzi.

"Utunzaji wa amani ni wajibu wa kila mwananchi katika taifa hili, hivyo kila mmoja wetu atumie muda wake kuitunza amani iliyopo," alisema. Mkurugenzi wa Uchaguzi ZEC, Thabit Idarous Faina, akiwasilisha mada kuhusu matayarisho ya Uchaguzi Mkuu 2020, alisema Tume hiyo tayari imeshafanya mambo mengi na kuchukua hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi ambazo zitawezesha kukamilisha uchaguzi huo kwa mafanikio makubwa.

Alisema, miongoni mwa mambo yaliyokamilika ni uandikishaji wa wapiga kura wapya na uhakiki wa taarifa za wapiga kura na jumla ya wapigakura 566,352 waliandikishwa.

Alisema, Tume ya Uchaguzi imefanya uteuzi wa wagombea 17 wa ngazi ya urais wa Zanzibar, wagombea 252 ujumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa majimbo mbalimbali ya uchaguzi na wagombea wa udiwani 360 kwa wadi zote.

Akizungumzia waangalizi wa uchaguzi, Faina alifafanua kuwa, Tume imeruhusu kuwapo kwa waangalizi wa uchaguzi katika Uchaguzi Mkuu 2020 na jumla ya taasisi 61 za ndani ziliomba kupatiwa vibali na zilizokidhi vigezo ni 35.

Alifafanua kuwa jumla ya taasisi 15 za kimataifa ambazo zimepatiwa vibali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) zimeomba pia kupatiwa kibali kuangalia uchaguzi wa Zanzibar.

Pia, mkurugenzi huyo alisema kwa mara ya kwanza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetumia bajeti yote ya uchaguzi bila kutumia pesa za wafadhili.

Alisema Tume ili kuhakikisha inaendesha uchaguzi huo bila ya kuwapo malalamiko, ilipitia upya matakwa ya sheria mpya ya uchaguzi, maelekezo ya miongozo juu ya majukumu kwa wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi na vituo pamoja na majukumu yao.

Hata hivyo, alisema wadau wa uchaguzi wanajukumu la kuhakikisha uchaguzi na harakati zake unakamilika kwa amani na Tume itakuwa karibu kufanya kazi nao kwa ushirikiano mkubwa ili kukamilisha kazi ya uendeshaji wa uchaguzi kwa salama na amani.



Mgombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM, Dk. Hussein Ali Mwinyi (wa pili kushoto), pamoja na viongozi wa dini na serikali wakiwa katika dua maalum ya kuliombea Taifa kuelekea kwenye uchaguzi mkuu wa amani katika uwanja wa kufurahishia Watoto Kariakoo, mjini Zanzibar jana. **PICHA: OMPR – ZNZ**

## Wenye ulemavu watakiwa kutumia haki yao

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kaskazini B Unguja, Rajab Ali Rajab, amewataka watu wenye ulemavu kushiriki katika kampeni za uchaguzi mkuu, ili wapate haki ya kusikiliza sera za wagombea bila ya kutengwa.

Aliyasema hayo Mahonda alipokuwa akikabidhi vifaa maalumu vya usaidizi kwa watu wenye ulemavu ambavyo vimetolewa na Taasisi ya Milele Foundation.

Alisema watakapoitumia fursa hiyo ya kusikiliza sera za wagombea watafanya maamuzi sahihi ya kuwachagua viongozi waowataka katika Uchaguzi Mkuu bila ya kushawishiwa.

Aliwataka waliokabidhiwa vifaa hivyo kuvienzi na kuvitunza ili viweze kuwasaidia katika shughuli zao za kila siku, na kuzitaka taasisi zinazosaidia watu wenye ulemavu kutochoka kufanya hivyo kwa watu wenye ulemavu kwa sababu wanahitaji misaada mbalimbali itakoyowarahisishia kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Naye mwenyekiti wa watu wenye ulemavu Wilaya ya Kaskazini 'B', Haji Khamis Nyange, aliitaka jamii isiwafiche watoto wenye ulemavu ili waweze kupatiwa haki zao za msingi.

Vifaa vilivyokabidhiwa ni pamoja na viti vya watu wenye ulemavu, magongo ya kutembelea, miwani ya jua, fimbo nyeupe, mabati na baiskeli za miguu mitatu.

# Dk. Shein anena kuhusu mafanikio ya Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kuwa mafanikio yanayoendelea kupatikana katika sekta ya miundombinu ni kielelezo cha kuyaendeleza Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwakomboa wananchi ili waweze kujiletea maendeleo ya uhakika.

Dk. Shein aliyasema hayo huko Kombeni wakati akiwahutubia wananchi katika hafla ya uzinduzi wa barabara ya Kombeni hadi Fuoni iliyokwenda sambamba na uzinduzi wa barabara ya Koani hadi Jumbi.

Alisema Mapinduzi ndiyo yaliyokomboa kila kitu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara na kila kitu cha maendeleo katika visiwa vya Unguja na Pemba kilianza baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964.

Akieleza historia ya miundombinu ya barabara, Dk. Shein alisema kuwa idara ya kazi ya barabara ndiyo iliyokuwa ikifanya kazi ya barabara mpya pamoja na zile za zamani baada ya Mapinduzi na baadaye ikabadilika na kuitwa Idara ya Ujenzi na Utengenezaji wa Barabara (UUB).

Alisema kuwa hatua ya ujenzi wa barabara hizo, pia ni miongoni mwa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015-2020 na kuipongeza Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa kusaidia utekelezaji wa ilani hiyo.

Alisema kuwa shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii zinategemea miundombinu ya barabara zilizo bora pia, juhudi za kuimarisha kilimo, utalii, uwezeshaji na sekta zote za kiuchumi kunahitaji kuwapo kwa barabara za kisasa.

"Nimefarajika kuona kwamba tumefanikisha kumalizika kwa barabara hizi tatu nilizoahidi kuzimaliza kabla ya muda wangu wa uongozi kwa nafasi ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kumalizika ambazo ni Fuoni-Kombeni, Koani-Jumbi kwa Unguja na Ole-Kengeja.

Pia, alisema kuwa faida zinazopatikana katika uendelezeji wa miundombinu ya barabara zinatokana na uamuzi uliochukuliwa na serikali wa kununua vifaa vipya vya ujenzi wa barabara vilivyogharimu Sh. bilioni 14.

Alihimiza Wakala wa Barabara kuwa na mipango imara ya kuzifanyia ukarabati barabara na kuwataka wafanyakazi wa Wakala wa Barabara kutofanya kazi kwa mazoea kwa kuwa serikali imo katika mchakato wa kuwaongezea mishahara ili walipwe vizuri.

Naye Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Dk. Sira Ubwa Mamboya, alisema uzinduzi wa barabara hizo ni hatua kubwa ya maendeleo iliyofikiwa katika uongozi wa Rais Dk. Shein wa Awamu ya Saba na zaidi ya kilomita 300 za barabara zimejengwa katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Mustafa Aboud Jumbe, alisema ujenzi huo ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020 kama ilivyoelezwa kwenye ukurasa wa 138 kifungu cha 83, kifungu kidogo cha b na c, Dira ya Maendeleo (Vision 2020), MKUZA III, Sera ya Taifa ya Usafiri pamoja na Mpango Mkuu wa Usafiri Zanzibar.

Mradi wa ujenzi wa barabara ya Kombeni hadi Fuoni yenye urefu wa kilomita 8.5 ni miongoni mwa nne ikiwamo ya Bububu, Chuini kuelekea Mahonda hadi Mkokotoni yenye urefu wa kilomita 31, Pale-Kiongele yenye kilomita 4.61, Matemwe-Muyuni Kilomita 7.58 Bububu Polisi hadi Chuini yenye urefu wa kilomita 2.8.

## HABARI PICHANI

# HEKA HEKA KAMPENI ZA UCHAGUZI MKUU




Aliyekuwa mbunge wa zamani wa CCM Jimbo la Temeke, Abbas Mtemvu (kulia), akimnadi mgombea udiwani katika Kata ya Miburani kupitia chama hicho, Juma Mkenga, Temeke Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mgombea ubunge wa Tandahimba kwa tiketi ya ACT- Wazalendo, Alphonce Hitu, akiomba kura katika mkutano wa kampeni uliofanyika Tandahimba mjini mwishoni mwa wiki. **PICHA: SAID POWA**



Mbunge mteule wa viti maalumu kupitia Umoja wa Vijana wa CCM, Asia Halamga, akiwaombea kura wagombea wa chama hicho, kwa nafasi ya urais, Dk. John Magufuli, ubunge wa Jimbo la Hanang', Mhandisi Samwel Hhayuma na udiwani Kata ya Ganana, Isaya Mbise, kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika soko la Ganana juzi. **PICHA: GIFT THADEY**



Wakereketwa wa CUF Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara wakiwashangilia viongozi wa chama hicho, waliopanda jukwaani kumnadi mgombea ubunge Jimbo la Masasi Mjini, Hamza Machuma katika mkutano wa kampeni hivi karibuni. **PICHA: HAMISI NASRI**




Aliekuwa mbunge wa viti maalumu Mkoa wa Arusha, Amina Mollel (kulia), akiendelea na kampeni za mtu kwa mtu wakati akiwaombea kura wagombea wa chama hicho, wa urais, ubunge na udiwani katika Soko la Ngaramtoni mwishoni mwa wiki. **PICHA: WOINDE SHIZZA**




Mama na mwanawe wakiwa wamejifunika bendera ya CCM, wakati wa uzinduzi wa kampeni za mgombea ubunge wa Jimbo la Ngorongoro kupitia chama hicho, katika Kijiji cha Misigyo hivi karibuni. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

HABARI KIMATAIFA

# Trump: Nitapona siku za karibuni

**Washington, MAREKANI**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amesema siku zijazo zitakuwa "mtihani halisi" katika kupona kwake maambukizi ya virusi vya corona.

Trump aliyasema hayo katika ujumbe wa video aliouweka kwenye ukurasa wa Twitter.

Video hiyo kutoka kwa Rais Trump, ambaye anatibiwa katika hospitali ya jeshi, inakuja baada ya taarifa zinazokinzana kusababisha mkanganyiko kuhusiana na hali yake kiafya.

"Nafikiri nitarejea hivi karibuni," alisema, na kuongeza kwamba anapambana kupona virusi hivyo kwa ajili yake binafsi na pia dunia kwa ujumla.

"Ni lazima nirejee kwa sababu bado tunapaswa kuifanya Marekani kuwa kubwa tena," alisema akitumia kauli mbiu ya kampeni yake.

Alisema anaanza kujisikia vizuri, lakini siku za hivi karibuni zitakuwa mtihani halisi wa kupona kwake, na amewashukuru waungaji mkono wake wa ndani ya nje ya nchi hiyo kwa kumtakia kupona haraka.

Daktari wake Sean Conley aliwaambia waandishi habari mapema kuwa hali ya Trump inaendelea vizuri na kusema timu ya madaktari ina furaha kubwa kwa maendeleo anayopitia rais."

Hata hivyo, chanzo kingine kimewaambia waandishi wa habari kwamba ishara muhimu za Trump zilikuwa zinatia wasiwasi.

"Ishara muhimu za rais katika muda wa saa 24 zilikuwa zinatia wasiwasi mno na saa 48 nyingine zitakuwa muhimu kwa maana ya huduma anayopewa.

Bado hatuko katika njia ya wazi kuelekea kupona kabisa, chanzo hicho kiliwaambia waandishi habari wa Ikulu ya Marekani ya White House wanaosafiri pamoja na rais.

Kituo cha televisheni cha FOX wakati huo huo kiliripoti kuwa Trump alionyesha hali ambayo si nzuri za kupona kutoka hali ya kawaida hadi mbaya kabla ya kupelekwa katika kituo cha afya cha Walter Reed, cha jeshi nje ya mji wa Washington, siku ya Ijumaa.

Hata hivyo, ripoti hiyo imemnukuu ofisa mwandamizi wa utawala huo akisema kwamba katika muda wa saa 12 zilizopita hakukuwa na wasiwasi kabisa.

Kumekuwa pia na ukosefu wa uwazi juu ya muda wa maambukizi ya rais huyo pamoja na lini alipimwa.

*DW*



Rais Donald Trump akinyoosha mkono kuonyesha ishara ya kuwa sawa kwa wanahabari (hawapo pichani) wakati anaelekea kuingia kwenye helikopta iliyompeleka hospitali. **PICHA: BBC**

## Mpinzani wa Kagame aendelea kusota jela

**Kigali, Rwanda**

MAHAKAMA ya Rwanda kwa mara nyingine imekataa ombi la kumwachiliwa kwa dhamana Paul Rusesabagina, anayejulikana kwa kuokoa maisha ya watu wengi wakati wa mauaji dhidi ya Watutsi na Wahutu wenye msimamo wa wastani mwaka 1994 wakati wa mauaji ya kimbari.

Mpinzani huyu wa Rais Paul Kagame, anakabiliwa na mashtaka 13, yote yakihusishwa na vitendo vya ugaidi.

Mahakama imeamua kwamba Paul Rusesabagina anaweza kutoroka nchi ikiwa ataachiliwa, kwa hivyo imefutilia mbali rufani dhidi ya ombi lake la dhamana.

Jaji pia alijibu hoja kadhaa zilizotolewa na upande wa utetezi, na pia familia ya Paul Rusesabagina, ambao wamebaini kwamba angelishtakiwa nchini Ubelgiji kwa sababu ya uraia wake wa Ubelgiji.

"Alizaliwa Mnyarwanda na hajapoteza uraia wake, kwa sababu inahitaji utaratibu wa kisheria," amesema jaji huyo, pia akibaini kwamba mahakama ya Rwanda ina uwezo wa kushughulikia kesi kwani uhalifu huo ulifanyike nchini Rwanda.

Paul Rusesabagina anahusishwa katika mashambulizi yaliyotekelezwa na kundi la FLN, tawi la kijeshi la kundi la MRCD, muungano wa vyama vya kisiasa vilivyo uhamishoni.

*RFI*

## Washukiwa mauaji ya kimbari mbaroni

**Kigali, Rwanda**

WATU watatu wanaoshukiwa kuhusika katika mauaji ya kimbari ya Rwanda mwaka 1994 wamekamatwa na kushtakiwa nchini Ubelgiji kwa ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu, ofisi ya mwendesha mashtaka ilisema Jumamosi. Ofisi hiyo haikutoa maelezo juu ya watu hao, lakini ilisema waliweza kutambuliwa kwa msaada wa maelezo ya mashuhuda wa nchini Rwanda katika uchunguzi uliofanywa na Ubelgiji.

Ofisi ya mwendesha mashtaka wa Rwanda baadaye iliwataja watatu hao kuwa ni Pierre Basabose, Seraphin Twahirwa na Christophe Ndangali na kutoa hati ya kimataifa ya kukamatwa kwao.

Mauaji ya kimbari ya mwaka 1994 yalipoteza maisha ya watu takribani 800,000, wengi wao wakiwa Watutsi lakini Wahutu wenye msimamo wa wastani.

*DW*

## Tshisekedi atuliza mambo Kivu Kusini

**DR Congo, BRAZAVILLE**

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Félix Tshisekedi, amewataka wananchi wake kuwa na subira baada ya balozi wa Rwanda kupuuzia mbali mauaji ya raia wa DRC eneo la Kasika, katika mkoa wa Kivu Kusini, mwaka 1998.

Balozi wa Rwanda Vincent Karega alikanusha kuhusika kwa wanajeshi wa Rwanda na kupinga yaliyomo kwenye ripoti iliyoitwa Mapping kama ilivyochapishwa na Kamisheni kuu ya UN.

"Hakuna hoja ya kumfukuza mwanadiplomasia huyo," alisema Rais Tshisekedi mbele ya waandishi wa habari wa DRC waishio Brussels, nchini Ubelgiji. Kauli ya rais imezua sintofahamu nchini humo.

Hakuna maana ya kuzusha uhasama," rais alisema. Félix Tshisekedi amebaini kwamba mchakato katika ngazi ya kidiplomasia umeanza kuishinikiza Kigali kumuonya Vincent Karega.

Kwa upande wa Seneta anayemuunga mkono Rais Kabila, Francine Muyumba, ambaye ameghadhibishwa kwa miezi kadhaa dhidi ya maneno yanayotolewa na wanadiplomasia wa kigeni jijini Kinshasa, alisema "Hatuwezi kufidia heshima ya taifa kwa kukidhi maslahi ya washirika."

Francine Muyumba ambaye ni mwenyekiti wa Tume ya ushirikiano katika Baraza la Seneti la DRC, alibaini kwamba Vincent Karega alifanya "kosa kubwa" ambalo

## Morocco, Marekani kushirikiana kijeshi

**RABAT, Morocco**

WAZIRI wa Ulinzi wa Marekani, Mark Esper aliyekuwa na ziara yake huko Afrika Kaskazini mwishoni mwa wiki. nchini Morocco, baada ya kuzuru Tunisia na Algeria wiki hii, amesema ziara hiyo ililenga kuimarisha ushirikiano wa kijeshi, vita dhidi ya makundi ya kijihadi na usalama katika kanda hiyo.

"Ushirikiano wetu uko imara na umedumu," Waziri wa Mambo ya Nje wa Morocco, Nasser Bourita amesema baada ya kukutana kwa mazungumzo na Waziri wa Ulinzi wa Marekani.

Mark Esper pia alikutana na mkuu wa majeshi ya Morocco na waziri wa ulinzi wa Morocco.

Kama ilivyokuwa nchini Tunisia, Septemba 30, Mark Esper alisaini mkataba wa miaka 10 ya ushirikiano wa kijeshi huko Rabat na Naibu Waziri anayesimamia Utawala na Ulinzi wa Kitaifa, Abdellatif Loudiyi, alibaini kwamba Marekani na Morocco zinafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu katika nyanja ya usalama.

Mkataba huu wa miaka kumi unafungua njia ya ushirikiano katika nyanja ya kimkakati ya kijeshi, ununuzi wa silaha na vifaa, mafunzo ya jeshi, na pia ujasusi kati ya nchi hizo mbili, ameripoti mwandishi wetu huko Casablanca, Nina Kozlowski.

**RFI**



# SARE YA CITY, LEEDS YAMRIDHISHA GUARDIOLA

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amekubali sare ya 1-1 yalikuwa matokeo ya haki kwa Manchester City baada ya kupata upinzani mkubwa kutoka kwa Leeds United pale katika dimba la Elland Road.

Raheem Sterling aliipa bao la uongozi City dakika ya 17, huku wakitawala mchezo wa kipindi chote cha kwanza, katika mchezo huo wa Ligi Kuu England, Jumamosi.

Hata hivyo, Leeds walipambana na kuweza kusawazisha bao hilo kupitia kwa Rodrigo baada ya makosa ya golikipa, Ederson.

Kipindi cha pili City walikabiliwa na upinzani mkubwa na walikoswa mara kadhaa kufungwa na Guardiola ameridhika na matokeo hayo, hasa kwa kuwa anawakosa wachezaji wake nyota.

“Ulikuwa mchezo mzuri na matokeo yalikuwa ya haki kabisa,” alisema Guardiola akiiambia Sky Sports.

“Tulicheza vizuri zaidi dakika 30 ambapo tulitakiwa kushinda mabao mengi, lakini hatukuweza.

“Tulijua kwamba hii ilikuwa ni timu ambayo muda wote inacheza kama fainali na tulitakiwa kujihami mapema.

“Lakini kwa timu yangu na hasa kutokana na hali halisi ilivyo, matokeo yale yalikuwa sawa kabisa kwa upande wetu na nimeridhika na kiwango cha timu yangu na wachezaji wangu.”

# Everton yafikia rekodi ya miaka 100 iliyopita

**LIVERPOOL, England**

EVERTON wanafurahia mwanzo bora zaidi wa msimu wa Ligi Kuu England kwa zaidi ya miaka 100 na wapo kwenye mbio za kuwania kushinda taji hilo ambalo mara ya mwisho walilibeba mwaka 1987.

Kikosi hicho cha kocha, Carlo Ancelotti kiliifunga Brighton and Hove Albion mabao 4-2 Jumamosi, yakifungwa na Dominic Calvert-Lewin, Yerry Mina na mawili ya James Rodriguez.

Toffees hao wameshinda mechi zao zote saba za mashindano yote tangu kuanza msimu huu 2020-21, mafanikio ambayo waliyapata msimu wa 1894-95.

Wamefunga mabao 24 katika mechi zote hizo, yakiwa mengi zaidi kuliko timu yoyote kwenye ligi tano kubwa za Ulaya.

Hii ni mara ya kwanza kwa Everton kushinda mechi saba mfululizo tangu msimu wa 1986-87, wakati walipotwaa ubingwa wa England kwa mara ya tisa na mara ya mwisho.

Wapo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England, wakiwa wameshinda mechi nne.

Mara ya mwisho Everton kushinda mechi nne mfululizo kwenye ligi hiyo ilikuwa ni msimu wa 1969-70, ambapo pia walishinda taji.

Calvert-Lewin ni mchezaji wa kwanza kufunga bao katika kila mchezo kwenye mechi nne za mwanzo za Everton msimu huu.



# KLOPP: LIVERPOOL INA NJAA YA MAFANIKIO

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp hana shaka kuhusu njaa ya Liverpool wakati kikosi hicho kikisaka tena mafanikio msimu huu.

Liverpool ilishinda taji la Ligi Kuu England kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1990 msimu uliopita na pia ilishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Vijana hao wa Klopp wameshinda mechi zao tatu za ufunguzi msimu huu na jana Jumapili walikuwa wanaikabili Aston Villa.

Kocha huyo wa Liverpool amesisitiza hana shaka na njaa ya mafanikio ya timu yake hiyo katika kutafuta mafanikio zaidi.

“Tumekubaliana kwamba, njaa ya mafanikio ndani ya kikosi chetu ni kubwa na kila mchezaji analijua hilo. Ndio maana wanacheza kwa bidii kubwa,” alisema Klopp.

“Sina shaka yoyote na molari ya wachezaji wangu na njaa waliyonayo kuhusu mafanikio ya uwanjani.

“Ni kazi ya kuhakikisha kwamba timu inafanya vizuri katika kila mchezo na kwa uhakika kabisa naliona hilo wazi kabisa.”

# LAMPARD

## AFUNGUKA NAMNA ANAVYOMTAKA HUDSON-ODOI



**LONDON, England**

FRANK Lampard amebainisha kwamba, Callum Hudson-Odoi bado yupo kwenye mipango yake pale Chelsea, licha ya kuhusishwa na kuwaniwa na Bayern Munich.

Kwa mujibu wa ripoti, Bayern ipo kwenye mazungumzo na Blues ili kumsajili kinda huyo wa Bavaria kwa mkopo kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili leo Jumatatu.

Hudson-Odoi alianza kwenye mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu England msimu huu 2020-21 wakati Chelsea ikiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Crystal Palace, Jumamosi.

Bayern kwa muda mrefu imeonyesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa England, Hudson-Odoi, lakini alisaini mkataba wa miaka mitano na Chelsea, Septemba, mwaka jana.


Hata hivyo, uwepo wa Christian Pulisic, Hakim Ziyech, Timo Werner na Kai Havertz ambao wameongezwa kwenye kikosi cha Lampard hivi karibuni umemfanya straika huyo kutokuwa na uhakika wa namba.

"Callum bado yupo kwenye mipango yangu hapa," alisema Lampard akiwaambia waandishi wa habari baada ya ushindi dhidi ya Palace.

"Tuna Pulisic na Ziyech, lakini tunahitaji machaguo zaidi kwenye winga.

"Alichokionyesha Callum leo, kinathibitisha kwamba anahitaji kuonyesha zaidi. Nimefurahishwa na kiwango chake.

"Kesho (leo Jumatatu) tutakuwa na majibu mazuri zaidi kumhusu yeye.



# HATIMA YA DEMBELE IPO MIKONONI MWAKE

**BARCELONA, Hispania**

RONALD Koeman amesema, Ousmane Dembele lazima aamue mwenyewe kuhusu majaliwa yake, huku kukiwa na uvumi wa kutakiwa Manchester United kutoka Barcelona.

United imeripotiwa kwamba inawaniwa kumsajili straika huyo wa kimataifa wa Ufaransa kwa mkopo, baada ya kushindwa kumsajili nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho.

Koeman alimwacha Dembele kwenye kikosi cha kwanza katika mchezo wa Alhamisi wakati Barca ikishinda 3-0 dhidi ya Celta Vigo na aliamua kuwachukua Pedri, Francisco Trincao na Ronald Araujo kwenye safu ya ushambuliaji.

Huku leo Jumatatu ikiwa ndio siku ya kufungwa kwa pazia la usajili barani Ulaya, Koeman amebainisha Dembele anaweza kuondoka kama anataka kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara.

"Siwezi kuzungumza sana kuhusu hili," alisema akiwaambia waandishi wa habari, Jumamosi.

"Mara zote nataka kupata kiwango bora kutoka kwa timu na wachezaji, lakini kama atabadilika, sitakuwa na sababu.

"Kama Pedri amecheza katika mechi mbili zilizopita ni kwa sababu ya kufanya vizuri kwenye mazoezi. Siku nyingine, Trincao na Pedri walipewa nafasi kwa sababu walistahili."

# Traore atarajia kuichezea Hispania

**MADRID, Hispania**

LUIS Enrique ana matumaini, Adama Traore ataichezea kwa mara ya kwanza Timu ya Taifa ya Hispania, licha ya kuitwa katika nchi yake ya asili ya Mali.

Winga huyo wa Wolves, Traore ana uhalali wa kuzichezea timu zote hizo mbili na zote zimemjumuishwa kwenye vikosi vyao kwa ajili ya mechi za kimataifa.

Hii ni mara ya tatu Hispania kumwita nyota huyo wa zamani wa Barcelona, lakini majeruhi na mlipuko wa virusi vya corona ukamfanya kushindwa kuichezea timu hiyo hadi sasa.

Lakini Enrique ambaye ni kocha mkuu wa timu ya Hispania ana imani Traore atakichezea kikosi hicho kwa mara ya kwanza.

"Hii ni mara ya tatu kuitwa, lakini hakucheza," alisema akiwaambia waandishi wa habari wakati akitangaza kikosi cha timu ya taifa.

"Ni mchezaji mwenyewe ndio anapaswa kuamua. Ninachokijua ni kwamba nimezungumza naye na anataka kuichezea Hispania."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# UNITED YAKARIBIA KUMSAJILI CAVANI

Straika huyo atua England kukamilisha vipimo vya afya na anatajwa ndiye mbadala wa ...

**MANCHESTER, England**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Paris St-Germain, Edinson Cavani, jana Jumapili alisafiri kwenda nchini England kwa ajili ya kujiunga na Manchester United.

Straika huyo wa kimataifa wa Uruguay mwenye umri wa miaka 33, amekuwa na mazungumzo ya muda mrefu na United na inadaiwa kwamba atajiunga na klabu hiyo kwa mkataba wa miaka miwili.

Cavani mkataba wake na Paris St-Germain ulimalizika Juni, mwaka huu na hivyo akawa mchezaji huru.

Aliondoka PSG baada ya kutokea kutoelewana na Neymar na huku akihisi kwamba ametosheka na soka la Ulaya.

United ilionyesha nia ya wazi ya kutaka kumsajili mchezaji huyo na ilikuwa ikifanya nae mazungumzo ya mara na kwa mara na sasa dili hilo linadaiwa kufikia sehemu nzuri hadi nyota huyo kukubali kusaini kwa mashetani wekundu hao.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka ndani ya Manchester United, umri wa Cavani sio tatizo kwao na kwamba, Kocha Ole Gunnar Solskjaer ana imani kubwa atakisaidia kikosi hicho kutokana na uzoefu wake.

Inaeleweka kwamba, mazungumzo na winga wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho yamekwama na hivyo United wanaona kama Cavani anaweza kuwa mbadala wake.

Cavani amefunga mabao 341 katika mechi 556 alizocheza huku pia akiweka reodi ya kufunga mabao 200 katika mechi 301 alizoichezea PSG na kuwa mfungaji bora wa wakati wote wa klabu hiyo.

Pia amefunga mabao 50 katika mechi 116 alizoichezea Timu ya Taifa ya Uruguay.

Kama dili hilo litakwenda kama lilivyopangwa, mmoja wa mchezo wa Cavani utakuwa dhidi ya timu yake ya zamani ya PSG, ambayo imepangwa kundi moja na United kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezo wao wa kwanza utapigwa Oktoba 20, mwaka huu, kwenye viunga vya Parc de Princes.

## KWA UFUPI

**ARSENAL YAMFUATA JORGINHO**
ARSENAL itaongeza nguvu ya kuwania kumsajili kwa mkopo kiungo wa Chelsea na Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 28, baada ya matumaini yao ya kumpata, Houssem Aouar wa Lyon mwenye miaka 22 kufifia. ***(ESPN)***

**SESSEGNON KUTUA BUNDESLIGA**
WINGA wa Tottenham Hotspur, Ryan Sessegnon mwenye umri wa miaka 20, anatarajia kujiunga kwa mkopo katika klabu ya Hoffenheim ya nchini Ujerumani. ***(Mail on Sunday)***

**WALCOTT AGOMBEWA EPL**
KLABU za Newcastle United, West Ham United na Crystal Palace zote zinawania saini ya nyota wa zamani wa England, Theo Walcott mwenye umri wa miaka 31 kutoka Everton. ***(Teamtalk)***

**TELLES AKARIBIA CITY**
MANCHESTER City inaweza kuizidi kete Manchester United katika mbio za kumsajili mlinzi wa kushoto wa Porto, Alex Telles mwenye umri wa miaka 27. ***(90Min)***

**CHELSEA YAIKATALIA BAYERN**
CHELSEA imekataa mpango wa Bayern Munich wa kutaka kumsajili winga wake, Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 19 kwa mkopo. ***(Mail on Sunday)***

**BAKAYOKO KUTUA NAPOLI**
KIUNGO wa Ufaransa, Tiemoue Bakayoko mwenye umri wa miaka 26, anatarajia kujiunga na Napoli kwa mkopo wa msimu mmoja kutoka Chelsea. ***(Mail Online)***

**GRACIA ATAKIWA BARCA**
BARCELONA imetoa ofa ya pauni milioni 13.6 ili kumsajili mlinzi wa kimataifa wa Hispania, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 19. ***(Mail Online)***

**PSG YAKOMAA NA ALLI**
KLABU ya Paris St-Germain imetoa ofa nyingine kwa Tottenham kwa ajili ya kumsajili kiungo wake, Dele Alli mwenye umri wa miaka 24, baada ya ile ya awali kukataliwa. ***(Sunday Telegraph)***

**UNITED, LIVERPOOL VITANI**
MANCHESTER United inakabiliwa na upinzani mkubwa kutoka kwa Liverpool katika mbio za kuwania kumsajili fowadi wa Barcelona, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 23. ***(Sport)***

**RUDIGER KUTUA AC MILAN**
AC Milan inawania kumsajili mlinzi wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Antonio Rudiger kwa mkopo wa muda mrefu, huku pia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 anawaniwa na Tottenham. ***(Calciomercato)***

**MOISE KUREJEA JUVE**
JUVENTUS ipo kwenye mazungumzo na Everton ili kumsajili tena, Moise Kean mwenye umri wa miaka 20, ambaye aliondoka kwa miamba hao wa Serie A mwaka 2019. ***(Corriere dello)***

**WATFORD YAMWANIA DOUGLAS**
KLABU ya Watford inawania kumsajili mlinzi wa Leeds United na Scotland, Barry Douglas mwenye umri wa miaka 31. ***(Football Insider)***



HABARI MICHEZO

# NYOTA WAGENI YANGA WAENDELEA KUNG'ARA

**Na Adam Fungamwango**

MABAO matatu yaliyofungwa na wachezaji wa kigeni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi, yameifanya timu yake Yanga kufikisha mabao saba ambayo yote yamefungwa na wachezaji kutoka nje ya nchi.

Mpaka kufikia raundi ya tano hakuna mchezaji yoyote wa Kitanzania aliyefunga goli kwenye mechi za Ligi Kuu kwenye timu hiyo.

Kwenye ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Coastal Union, mabao yalifungwa na Carlos Carlinhos mchezaji kutoka nchini Angola, Haruna Nyonzima ambaye ni Mnyarwanda na Yacouba Songne anayetokea Burkina Faso.

Kwenye mechi ya kwanza, Yanga ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Tanzania Prisons, bao likifungwa na raia wa Ghana, Michael Sarpong, huku mechi ya pili ikicheza dhidi ya Mbeya City na kushinda goli 1-0, shukrani kwa beki, Lamine Moro ambaye naye ni raia wa Ghana. Nyota huyo Mghana pia alifunga bao kwenye mechi ambayo Yanga ilicheza dhidi ya Mtibwa Sugar, ikishinda bao 1-0.

Bao lingine la Yanga lilifungwa na Mkongomani Tonombe Mukoko aliyefunga bao pekee kwenye mechi dhidi ya Kagera Sugar, ikitoka na ushindi wa goli 1-0.

Ni tofauti kidogo na watani zao wa jadi Simba ambao wana mchezaji Mtanzania ambaye tayari ameshafunga magoli, ingawa nao wana idadi kubwa ya wageni waliofunga mabao.

Mbongo pekee wa Simba waliyetumbukiza mpira wavuni ni kiungo, Mzamiru Yassin ambaye ana mabao mawili mpaka sasa aliyofunga kwenye mechi ya kwanza dhidi ya Ihefu, timu hiyo ikishinda mabao 2-1, lakini kwenye mechi dhidi ya Mtibwa Sugar, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1.

Yanga sasa imefikisha pointi 13, ikicheza mechi tano, kushinda nne na kutoka sare mara moja, ikifunga mabao saba na kufungwa moja.



Wachezaji wa Yanga wakishangilia moja ya magoli waliyofunga katika mechi ya Ligi Kuu Bara, dhidi ya Coastal Union iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi usiku. Kutoka kushoto ni Yacouba Sogne, Mukoko Tonombe, Haruna Niyonzima na Adeyum Ahmed. Yanga ilishinda mabao 3-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Prisons, City walia na mastraika

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mechi ya 'dabi' ya Nyanda za Juu Kusini ikimalizika juzi kwa suluhu, makocha wa timu hizo wamelalamikia safu zao za ushambuliaji kuwa ndizo zilizosababisha mechi hiyo kumalizika hivyo.

Kocha Mkuu wa Mbeya City, Amri Said, amesema kuwa bado safu yake ya ushambuliaji imekuwa dhaifu, huku Salum Mayanga ambaye ni Kocha Mkuu wa Prisons akisema alitengeneza nafasi nyingi, lakini walishindwa kuzitumia vizuri.

"Kwanza kabisa niliwatengeneza wachezaji wangu kisaikolojia baada ya kupoteza mechi zote tulizocheza. Siku zote 'dabi' ni ngumu sana, pointi moja si mbaya ila najua timu yangu ina udhaifu kwenye utafutaji magoli, hilo bado nalifanyia kazi," alisema Amri.

Beki huyo wa zamani wa Simba na Majimaji alikisifu kikosi chake kwenye nafasi ya ulinzi na kiungo kuwa ilicheza vyema na kubadilika tofauti na mechi zilizopita.

"Ukiangalia kipindi cha kwanza tulikamata dimba, kipindi cha pili ndiyo tulipotea na hii ni kutokana na mfumo niliyowaambia wachezaji wengi wacheze kipindi cha pili, uliwatatiza, lakini kwangu mimi pointi moja nimeipokea kwa mikono miwili," alisema kocha huyo.

Kwa upande wa Mayanga alisema timu yake iliingia kwa tahadhari, lakini baadaye walifanya mashambulizi kadhaa na kupata nafasi ambazo walishindwa kuzitumia.

"Tulipata nafasi kadhaa tumeshindwa kuzitumia, lakini hii ndiyo 'dabi' yenyewe," alisema Mayanga.

## Mgunda azibeba lawama Coastal

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kufungwa mabao 3-0 na Yanga katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam, Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, amesema lawama za kichapo hicho anazibeba yeye na si mtu mwingine yoyote.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mgunda alisema wachezaji wake wamekuwa wakifanya makosa ambayo yanajirudia jambo ambalo halimfanyi kuwalaumu na kuendelea kuyafanyia kazi.

**Mgunda alisema imekuwa ni kawaida kwa wachezaji wake kupoteza umakini na kufanya makosa yanayofanana jambo ambalo amepanga kulitafutia 'dawa'.**

"Ni kweli tumefungwa mabao ya kujirudia rudia, ila kwa mabao hayo hayatanifanya niwalaumu wachezaji wangu, wapo vizuri na uwezo wanao ila tatizo lao ni kwamba wanafanya makosa ambayo yanajirudia, hili linaniumiza sana," alisema Mgunda.

Kocha huyo alisema kuna wakati analazimika kutumia nguvu kubwa kuongea na wachezaji wake hadi sauti inakauka ili kuhakikisha wanafanya vizuri, lakini mambo yanakwenda tofauti.

"Sitachoka kuongea nao, nina imani baada ya muda kikosi changu kitakuwa vizuri na kitaimarika zaidi na kupata matokeo mazuri katika mechi zetu zijazo," Mgunda alisema.

## KMC yaitangazia 'hatari' Polisi TZ

**Na Saada Akida**

RAUNDI ya tano ya Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kukamilika leo kwa Kikosi cha Manispaa ya Kinondoni maarufu KMC FC kuwakaribisha Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa KMC, Christina Mwagala, aliliambia gazeti hili kuwa timu yao imejiandaa vyema kuelekea mchezo huo na wanaamini kasi yao ya ushindi itarejea.

Mwagala alisema wachezaji wao wameahidi kuutumia vizuri uwanja wa nyumbani na wamerekebisha makosa yaliyojitokeza katika mechi iliyopita.

"Kila kitu kinakwenda vizuri, kikosi chetu kinachonolewa na Kocha Mzawa, Habibu Kondo kinawataka Polisi wajipange kwa mchezo wa kesho (leo), kwa kifupi tuna zawadi ambayo wamewaandalia mashabiki wetu," alisema Mwagala.

Alisema wamefanya mazoezi ya kiwango cha juu na wako tayari kutimiza ahadi ya kuondoka na ushindi katika mechi hiyo.

"Tumejipanga vizuri na hakuna mchezaji mwenye majeraha, kikosi kipo tayari kupambana kusaka ushindi, mchezo wa kesho (leo), utaturudisha kwenye kasi ya kutokufungwa kila mechi, na hivyo kuwapa furaha mashabiki wetu," aliongeza kiongozi huyo.

Michezo
Jumatatu Oktoba 5, 2020
Nipashe



## UNITED YAKARIBIA KUMSAJILI CAVANI

HABARI UK 22

## MJERUMANI ATUA KUWANOA YANGA

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Yanga unatarajia kumtangaza kocha wa zamani wa Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, Ernst Middendorp kuchukua mikoba ya Mserbia, Zlatko Krmpotic ambaye kibarua chake cha kuifundisha timu hiyo kilimalizika juzi usiku, imefahamika.

Middendorp naye alitimuliwa katika nafasi ya ukocha wa Kaizer Chiefs tangu Septemba 10, mwaka huu na Kocha wa Bidvest Hunt alitangazwa kuchukua mikoba yake siku tisa baadaye.

Middendorp alitua kwa vigogo hao wa Soweto Desemba, mwaka 2018 akichukua nafasi ya Giovanni Solinas, ikiwa ni mara ya pili anaiongoza timu hiyo.

Taarifa rasmi iliyotolewa na Yanga inasema wamevunja mkataba baada ya pande mbili kufikia makubaliano.

"Uongozi wa Yanga unapenda kuwataarifu mashabiki, wapenzi na wanachama wa Yanga, pamoja na wadau kuwa klabu imefikia makubaliano na mwalimu, Zlattko Krmpotic ya kusitisha mkataba wake mara moja, klabu inapenda kumtakia Zlatko kila la kheri katika shughuli zake kwingineko," ilisema taarifa ya Yanga.

Krmpotic aliiongoza Yanga kwa siku 37, akichukua mikoba iliyoachwa na Mbelgiji, Luc Eymael aliyefukuzwa pia Agosti, mwaka huu.

Kocha huyo aliiongoza Yanga katika mechi tano za mashindano, ameshinda nne na kutoka sare mchezo mmoja.



Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere (kulia), akijaribu kumtoka beki wa JKT Tanzania, Edson Katanga katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma jana. Simba ilishinda mabao 4-0. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YATUMA SALAMU YANGA

●●●Yaishusha kileleni baada ya kuichapa JKT Tanzania mabao 4-0, huku ikicheza kandanda safi...

**Na Adam Fungamwango**

MAGOLI mawili yaliyofungwa na straika hatari wa Simba, Meddie Kagere, na moja ya Chriss Mugalu na lingine kutoka kwa Luis Miquissone yaliifanya timu hiyo jana kuibuka na ushindi mnono wa mabao 4-0 katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana.

Kwa matokeo hayo Simba imefikisha pointi 13 na kuishusha Yanga yenye pointi sawa kileleni, kabla ya mechi ya jana usiku kati ya Azam FC dhidi ya Kagera Sugar.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara wameiteremsha Yanga kutokana na kuwa na faida ya mabao ya kufunga, huku kila timu ikiwa imecheza mechi tano, kushinda nne na sare moja.

Ilikuwa ni kama kujibu mapigo ya watani zao wa jadi, Yanga ambao waliitwanga Coastal Union mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam juzi.

Karamu ya mabao ilianza mapema dakika ya tatu tu ya mchezo, Kagere alipoipatia Simba bao la kwanza, alipounganisha kwa kichwa mpira wa krosi iliyochongwa na Rarry Bwalya.

Kabla JKT Tanzania hawajakaa vizuri dakika tatu baadaye, Mugalu aliiandikia Simba bao la pili, akifunga kwa kichwa kama mwenzake kutoka upande ule ule ya winga ya kulia, lakini safari hii krosi ilichongwa na Miquissone.

Dakika ya tisa nusura JKT Tanzania wapate nao, baada ya faulo iliyopigwa na Michael Aidan kuzua kizaazaa langoni mwa Simba na mpira ukagonga mwamba, kabla ya kuokolewa na mabeki wa Simba.

Mugalu aliikosesha Simba bao dakika ya 19 aliposhindwa kuunganisha krosi ya Kagere, huku Claotus Chama naye akikosa bao la wazi dakika ya 34 alipowalamba chenga mabeki wa JKT Tanzania, lakini akiwa anatazamana na lango alipiga shuti kubwa lililopaa juu.

Alikuwa ni Kagere tena, kwenye dakika ya 40 alipoifungia Simba bao la tatu kwa shuti kali la mguu wa kushoto kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na Bwalya aliyepiga krosi kutoka winga ile ile ya kulia, ukamkuta Chama ambaye alimtengenezea mfungaji aliyeukwamisha wavuni na kumwacha kipa Patrick Muntary akiwa hana la kufanya.

Alikuwa ni Miquissone dakika ya 53 alipopigilia msumari kwenye jeneza la JKT Tanzania, baada ya kuipatia Simba goli la nne na kuzima ndoto za maafande hao kuzoa pointi hata moja kwenye uwanja wao wa nyumbani.

Kagere aliunganisha krosi kutoka kwa Chama, lakini mpira huo uliokolewa na mabeki wa maafande hao na kwenda kiasi cha miaka 35 hivi ukakutana na Miquissone ambaye aliachia kombora kali la juu lililokwenda moja kwa moja hadi wavuni na kumuacha kipa Muntari akiutazama tu.

Simba ilifanya mabadiliko kwa kuwatoa Kagere, Miquissone na Chama, nafasi zao zikachukuliwa na Mzamiru Yassin, Hassan Dilunga na Benard Morrison, ambayo yaliyonekana zaidi ni ya kulinda ushindi kuliko kutafuta mabao mengine.

Pia baada ya mabao hayo, ilionekana wachezaji wa Simba waliridhika na kuanza kucheza mpira wa kuwafurahisha mashabiki zaidi.

JKT Tanzania yenye pointi nne iko katika nafasi ya 16, ikicheza mechi tano, kushinda moja, sare moja, ikipoteza michezo mitatu, ikifunga mabao mawili tu na kufungwa magoli nane.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002